

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 3 Septemba, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Ulimbwa)

DUA

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu

*(Mheshimiwa Mbunge aliyetajwa hapo juu aliapa
kiapo cha uaminifu)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kwa niaba yenu naomba tumkaribishe Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki. Sasa wananchi wa Singida Mashariki wanae mwakilishi halali Bungeni. Ningependa pia kuwataarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko safari na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa wakati huu ni Mheshimiwa William Lukuvi. *(Makof)*

Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada mitatu ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

Kwanza Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali kwa Mwaka 2019 (*The Appropriation Bill, 2019*). Pili, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (*The Finance Bill, 2019*). Tatu, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2019, (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 3, 2019*).

Kwa Taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo mitatu imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi, zinazoitwa; Kwanza, Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali Na. 7 ya Mwaka 2019 (*The Appropriation Act, No. 7 of 2019*). Pili, Sheria ya Fedha Na. 8 ya Mwaka 2019 (*The Finance Act, No. 8 of 2019*) na Tatu, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3, Na. 9 ya Mwaka 2019, (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 3, Act No. 9 of 2019*).

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaendelea na utaratibu wetu wa maswali na wale mtakaopata nafasi ya maswali ya nyongeza, utaratibu wetu ni uleule swali liwe fupi linalouliza kuhusu kitu kimoja na ambalo linaanza na kuuliza. Linaanza na *question mark*, itakuwa bora zaidi. Naomba nimuite Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa, endelea.

Na. 1

**Azimio Kuhusu Faida Inayotokana na Demografia Iliyopo
kwa Kuwekeza kwa Vijana**

MHE. RICHARD P. MBOGO (K.n.y JAMAL KASSIM ALI)
aliuliza:

Mwaka 2017, Umoja wa Afrika (*AU*) ulipitisha Azimio kwa nchi za Afrika la kuhakikisha kuwa nchi hizi zinavuna faida itokanayo na Demografia iliyopo kwa kuwekeza kwa vijana:-

(a) Je, Serikali ya Tanzania imechukua hatua gani katika utekelezaji wa Azimio hilo?

(b) Je, ni mafanikio gani yamepatikana kama nchi baada ya utekelezaji huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI,VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha 29 cha Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kilicofanyika Mjini Addis Ababa kiliweka Azimio Na. 601 lilitangaza mwaka 2017 kuwa ni mwaka wa "Kuvuna Faida itokanayo na Demografia kuitia Uwekezaji kwa Vijana" (*Harnessing the Demographic Dividend Through Investments in Youth*).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azimio hilo Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kutoa mikopo ya kuwawezesha vijana kuanzisha na kuendelea miradi yao ya uzalishaji mali kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ambapo katika kipindi cha mwaka 2014/2015 hadi 2019 Serikali imewezesha vikundi vya

vijana 755 ambavyo vimepatiwa mikopo ya shilingi bilioni 4.2 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

(ii) Kurekebisha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 ya Mwaka 2017 inayozitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha asilimia 10 kutokana na mapato yao ya ndani kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa ajili ya mikopo.

(iii) Kuibua bunifu 31 za vijana katika Sekta ya Sayansi na Teknolojia. Kati ya hizo, bunifu 11 zimefanyiwa tathmini ya kisayansi na kwa sasa ziko katika hatua mbalimbali ikiwemo kuwekwa kwenye kiota atamizi (*incubator*) kabla ya hatua ya majaribio ya uzalishaji.

(iv) Kutoa mafunzo ya ufundu stadi kwa vijana 5,875 kupitia taasisi ya Don Bosco *Net Tanzania*, kurasimisha ujuzi wa vijana 10,000 waliouopata nje ya mfumo rasmi ya mafunzo kupitia *VETA* na Serikali kwa kushirikiana na waajiri imeibua fursa 1,800 za mafunzo ya vitendo mahali pa kazi, ambapo wahitimu 292 wameshapelekwa kuanza mafunzo.

(v) Kutoa mafunzo maalum ya vitalu nyumba kwa Halmashauri zote nchini ili kufikia vijana wasiopungua 18,000, tayari Mikoa 12 imeanza programu hii kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa Azimio hilo mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Ongezeko la ajira kwa vijana katika sekta binafsi;

(ii) Ongezeko la vijana wanaojitegemea kutokana na kujajiri wao wenye;

(iii) Ongezeko la vijana wenye ujuzi wa kujajiri na kuajiriwa; na

(iv) Upatikanaji wa mikopo yenne masharti nafuu kwa vijana.

SPIKA: Mheshimiwa Mbogo, nimekuona swali la nyongeza.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, tunajua Muungano wa Kikanda au wa Kimataifa kama vile *SADC* una faida kubwa nzuri sana kwa vijana hususan kwenye kupata ujuzi pamoja na mafunzo. Je, huu mkutano uliopita hivi karibuni nini vijana watafaidika na *SADC*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuna maazimio gani ambayo tayari yaliyopo aidha kwenye *EU* umoja mwingine wa Kimataifa ambayo yatasaidia vijana zaidi kwenye suala lile la mikopo

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye Mkutano wa *SADC* uliomalizika hivi karibuni tuchukue fursa hii kuwashukuru sana Wakuu wote wa nchi pamoja na Mwenyekiti wetu wa *SADC* kwa azma na kauli yao thabiti ya kuhakikisha kwamba vijana wanashiriki katiak sekta ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano uliomalizika agenda kubwa ilikuwa ni kuwashirikisha vijana katika uchumi wa viwanda na kwa Tanzania vijana walipata fursa ya kutembelea na kuona fursa mbalimbali na kujifunza kuitia Mataifa mengine na tunaamini kabisa kuitia Mkutano huu liko jambo ambalo limeongezeka katika fikra za vijana hasa katika kwenda kuwekeza kwenye uchumi wa viwanda. Kwa hiyo ni Mkutano ambao ulikuwa na tija na vijana wamehamasika na tunaamini kutokea hapo vijana wengi

zaidi watashiriki katika uchumi wa viwanda, moja kwa moja au isivyo moja kwa moja.

Mhehsimiwa Spika, swali lake la pili alitaka kujuua Maazimio ya Kikanda kupitia AU. Katika Azimio la 601 la mwaka 2017 katika moja ya nguzo iliyosemwa ni uwezeshwaji wa vijana na Serikali ya Tanzania tunayafanya hayo kupitia Mifuko mbalimbali ya Uwezeshaji wa Vijana na kuwajengea vijana uwezo hasa katika kuwajengea ujuzi ili waweze kujajiri na kuajiri vijana wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali ya Awamu ya Tano inayafanya hayo kuzingatia maamuzi yaliyofikiwa na Wakuu wa nchi katika Umoja wa Afrika.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Waheshimiwa Wabunge. Swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula.

Na. 2

Hitaji la Jenereta Hospitali ya Mkoa – Geita

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA (K.n.y JOSEPHINE T. CHAGULA) aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Geita haina jenereta la dharura pindi umeme unapokatika na hivyo kusababisha vifo vingi kutokea:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka jenereta la dharura katika hospitali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jenereta lililokuwa linatumika katika hospitali ya Mkoa wa Geita lilipata hitilafu na hivyo kufanya hospitali ya Mkoa wa Geita kutokuwa na jenereta la dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hospitali ya Mkoa wa Geita imepata jenereta mbadala lenye ukubwa wa KVA 400 ambalo linakidhi mahitaji yote ya hospitali. Jenereta hili lilitpatikana kutoka Halmashauri ya Mji wa Geita kuititia Mgodi wa GGM.

SPIKA: Mheshimiwa Lolesia.

MHE. LOESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, kwanza nilipongeze sana Serikali kwa kupeleka jenereta tena kwa ajili ya kuendeleza huduma katika hospitali ya Mkoa wa Geita, lakini bado kuna changamoto nyingine pia kwamba hospitali ya Mkoa wa Geita pia ina upungufu mkubwa sana wa watumishi. Je, Serikali inasemaje kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama ilivyo hospitali ya Mkoa wa Geita pia katika vituo vingi vya kutolea huduma kwenye Mkoa wa Geita hakuna nishati ya umeme na hii inasababisha huduma kutolewa lakini pia kupata changamoto hasa kwa akina mama wajawazito wakati wa kujifungua usiku;

Je, Serikali inasemaje kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinapatiwa huduma ya umeme maeneo yote katika Mkoa wa Geita. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Dkt. Faustine Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli

tunakiri kwamba katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita tuna changamoto ya rasilimali watu, watumishi waliokuwepo pale ni takriban asilimia 50 ya watumishi wote ambaao wanahitajika. Serikali imeliona hilo na inaendelea kuongeza watumishi kadri vibali vya ajira vinavyopatikana. Sambamba na hilo, tunaendelea kusomesha wataalam mbalimbali kuhakikisha kwamba zile huduma za kibingwa basi zinapatikana katika Mkoa huu wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameulizia kuhusu suala la umeme katiak vituo vyetu vya kutolea huduma za afya. Wizara ya Afya tumekuwa tunafanya kazi kwa karibu sana na Wizara ya Nishati kuititia mpango wa *REA* na moja ya mkakati katika mradi huu ni kuhakikisha kwamba vituo vyote vya kutolea huduma za afya na shule vinapata umeme. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Afya kushirikiana na Wizara ya Nishati kuititia mradi wa *REA* itahakikisha kwamba maeneo yote ambayo yanapitiwa na mradi wa *REA* basi nayo yanapata umeme.

SPIKA: Tunaendelea na swali la pili kwa Wizara ya Afya, litaulizwa na Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 3

Kuongeza Madaktari Bingwa Nchini

MHE. SONIA J. MAGOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Madaktari Bingwa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jin sia, Wazee na Watoto, naomba

kujibu swalii la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za kibingwa katika ngazi mbalimbali za huduma nchini ikiwa ni pamoja na hospitali yetu ya Taifa Muhimbili. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ilitenga kiasi cha shilingi bilioni Mbili zilizotumika kwa ajili ya kusomesha Madaktari Bingwa 125 wa fani za kipaumbele katika Chuo cha Muhimbili (*MUHAS*) ambao wanatarajia kukamilisha masomo yao mwaka 2020/2021. Aidha, katika mwaka 2018/2019, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1.8 ili kuendelea kugharamia mafunzo ya ngazi ya kibingwa katika kada mbalimbali za afya 127 katika Chuo cha *MUHAS*.

Aidha katika mwaka 2018/2019 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1.8 ili kuendelea kugharamia mafunzo ya ngazi za bingwa kwa kada mbalimbali za afya 127 katika Chuo cha *MUHAS*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2019 jumla ya watumishi wa sekta ya afya 458 walikuwa wanaendelea na masomo katika ngazi mbalimbali za taaluma kwa idadi hiyo, 435 wanaendelea na masomo yao ndani ya nchi na 23 nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali; katika idadi hiyo, jumla ya madaktari bingwa 365 wanatarajiwa kuhitimu mafunzo kuanzia mwaka 2019/2020, 2020/2021, 2021/2022. Wataalam wote hawa watasambazwa katika hospitali mbalimbali nchini kulingana na uwiano wa wataalam waliopo na kwa kuzingatia maeneo yenye uhaba mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 Wizara imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya watalaam bingwa katika fani za kipaumbele. Kutokana na uhaba uliopo katika hospitali za rufaa za mkoa Wizara itahakikisha fedha hizi zinatumika vyema katika kusomesha wataalam wanaotoka katika maeneo yenye uhaba mkubwa. Aidha Wizara kuititia hospitali za rufaa za

Taifa na taasisi za nje inaendelea kuendesha kambi za udaktari bingwa hapa nchini kwa lengo la kusogeza huduma za kibingwa na kuwajengea uwezo wataalam wetu.

SPIKA: Mheshimiwa Sonia ameridhika, hana nyongeza.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, asilimia kubwa ya wananchi wetu kipato chao ni cha chini na wamekuwa wakitegemea hpspitali zetu za Serikali kama msaada mkubwa pindiwanapopata changamoto za afya. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba, hawa madktari bingwa wachache ambao tunao hawapati vishawishi vya kwenda kufanya kazi nje ya nchi ama kwenye *private hospitals*?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; ukiangalia idadi ya madaktari bingwa ambao tunao bado ni chache sana, lakini hospitali nyingi za mikoa hazina madaktari bingwa. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha madaktari hawa wanagawiwa kwa uwiano mzuri, ili kuepusha usumbufu wa Wananchi wengi kutoka mikoani na kufuata huduma Hospitali ya Muhimbili? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Afya, Dkt. Ndugulile, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako kwamba, katika nchi ambazo tumejaliwa kidogo kwamba, madaktari wetu hawatoki sana kwenda nje ya nchi kulinganisha na nchi nyingine katika Bara la Afrika, Tanzania ni mojawapo.

Mheshimiwa Spika, na moja ya mkakati ambao tumeuweka wa kuhamasisha madaktari wetu na wataalam wetu wa afya kuendelea kukaa nchini ni maboresho ambayo

tunaendelea kuyafanya katika sekta ya afya; vituo zaidi ya 352 tumeviboresha, hospitali za wilaya 67 tumejenga, sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa hospitali za rufaa tano za mikoa na maboresho mengine makubwa ya kimiundombinu, ya vifaa, ambayo sasa hivi yamesababisha kwamba, hata huduma zile kubwa za kibingwa ambazo zilikuwa zinafanyika nje ya nchi sasa hivi zimeweza kufanyika nchini. Kwa hiyo, hili nalo limesaidia sana kuwafanya wataalam wetu wazalendo kubaki, pamoja na motisha nyingine za ndani ambazo tumeendelea kuwapatia watalaam wetu katika sekta yetu ya afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sonia Magogo ameulizia suala la uwiano; ni kweli tunakiri tumekuwa na changamoto kubwa sana ya uwiano wa upatikanaji wa Madaktari Bingwa katika baadhi ya mikoa. Na hili sisi kama Wizara tumeshalliona na moja ya mkakati ambao tumeufanya sisi kama Wizara ni kuhakikisha kwamba, wataalam ambao tunaenda kuwasomesha kwa fedha ya Serikali tunachukua katika maeneo ambayo yamekuwa na uhaba mkubwa wa wataalam kwa lengo kwamba akimaliza na tumewasainisha kitu kinaitwa *bonding* kwamba, ukimaliza na iwapo kama umesoma na fedha za Serikali basi tutakurudisha kulekule katika maeneo ambayo ulikuwa umetoka, ili uweze kupata utaalam huo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha mpito ambapo huduma hizi hazijaweza kupatikana katika baadhi ya mikoa ndio tumekuwa tunaendesha kambi; Madaktari Bingwa hawa wachache tulio nao tumekuwa tunawazungusha ndani ya nchi kwa kambi maalum katika baadhi ya mikoa, ili waweze kutoa himo huduma kwa wale Wananchi, ili angalau katika ile mikoa basi huduma zile ziweze kupatikana.

SPIKA: Wizara ya Maji, swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi. Nimekuona Mheshimiwa, kwa niaba yake.

Na. 4

Chanzo cha Maji cha Sigaleti – Ruaha

MHE. CONCHESTER RWAMLAZA (K.n.y MHE. JOSEPH L. HAULE) aliuliza:-

Aliyekuwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng*, Isack Kamwelwe, alitembelea chanzo cha maji cha Sigaleti kilichopo Kata ya Ruaha ambacho kimepimwa na kuthibitishwa na Wataalam wa Idara ya Maji kwamba, kina maji mengi na salama na kinawenza kuhudumia ipasavyo Kata za Ruaha, Kidodi na Ruhembe. Na kwamba, zinatakiwa shilingi billioni 2 ili maji hayo yaweze kupatikana kwenye kata hizo:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga kiasi cha fedha kwenye bajeti, ili kuokoa maisha ya wananchi zaidi ya 35,000?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Ruaha, Kododi na Ruhembe ni mionganoni mwa kata 18 zilizopo katika Jimbo la Mikumi. Upatikanaji wa huduma ya maji katika Jimbo hilo umefikia asilimia 68.

Mheshimiwa Spika, Kata za Ruaha, Kidodi n Ruhembe zina jumla ya vijiji 12, hata hivyo vijiji vinane tayari vimejengewa miundombinu ya miradi ya bomba; aidha vijiji vinne katika Kata ya Ruhembe vinatumia visima vifupi vilivyofungwa pampu za mkono, hivyo uboershaji wa huduma ya maji katika kata hizo bado ni muhimu kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wakazi na kukua kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli chanzo cha maji cha Mto Sigaleti ni miongoni mwa vyanzo vya maji vinavyopendekezwa kutumika kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Jimbo la Mikumi, zikiwemo kata hizo. Baada ya kupata makisio ya awali ya kiasi cha shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo, kwa sasa Wizara yangu inafanya mapitio ya kina ya usanifu na alama na tayari kiasi cha shilingi milioni 658 kimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

SPIKA: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza nimekuona.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, sasa Serikali imetenga pesa kama ilivyo katika majibu ya msingi. Na kwa kuwa, tatizo la maji katika Kata zilizotajwa katika swali hilo ni ya muda mrefu. Je, Serikali inajili-*commit* vipi kwamba, huu mradi wa kuweka maji katika kata hizo utakamilika wakati gani?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba, kumekuwa na matatizo makubwa sana katika miradi ya maji katika nchi yetu na Serikali inaahidi kutoa pesa kwenye bajeti, lakini fedhahaziendi kama inavyotarajiwa, lakini pia hata fedha zinazoenda zinatumika vibaya na kuifanya miradi hii isikamiliike. Je, Serikali sasa inachukua hatua zipi kuhakikisha kwamba, hii miradi ya maji ambayo inapata fedha za Serikali inakamiliika na fedha zinatumika ipasavyo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwanza sisi kama Serikali tumefanya jitihada kubwa sana pale Mikumi Mjini. Zaidi ya mradi wa milioni 974

tumeweza kutekeleza kupitia chanzo cha Madibira katika kuhakikisha wananchi wale wanapata huduma ya maji, lakini katika kuhakikisha tunatumia chanzo hiki cha Sigaleti sisi tunapitia usanifu kwa mara ya mwisho kabisa. Na ninataka nimhakikishie sisi kama Wizara ya Maji tutafanya jitihada kuhakikisha mradi huu tunauanza na kutekeleza katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kumtua mwanamama ndoo kichwani inatimilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Na sisi kama Serikali, Serikali inatupa fedha moja ya changamoto kubwa ilikuwa ni muundo, lakini kupitia Bunge lako Tukufu umetunga sheria katika kuhakikisha kwamba, tuna sheria Namba 5 ya Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira na Uanzishwaji wa Wakala wa Maji *RWASA*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge huu utakuwa muarobaini katika kuhakikisha usimamizi wa miradi ya maji na fedha, kwa maana ya wakandarasi katika kuhakikisha wanatekeleza miradi ya viwango na katika kuhakikisha tunatatu matatizo ya maji, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza tafadhali? (*Makofii/Vigelegele*)

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kunijalia kuingia kwenye Bunge lako Tukufu na kuweza kuwawakilisha ipasavyo Wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ikungi pamoja na Jimbo la Singida Mashariki ni kama ambavyo swali la msingi liliyoyouliwa lina matatizo yanayofanana na jimbo liliyoyouliwa katika swali la msingi. Pamoja na matatizo hayo zimefanyika jitihada, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya kipenzi chetu Dkt. John Pombe Magufuli, wameshatuletea takribani bilioni 1 na milioni 500 kuchimba visima virefu 28.

Mheshimiwa Spika, sasa nimekuja hapa kuomba kwa kupitia Waziri, wako tayari, tumeshafanya tathmini ya kutosha tuweze kupata, maana kuchimba maji na kuyapata ni jambo moja na kutoka maji ni jambo la pili. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba, kupitia tathmini iliyoofanyika na iko Wizarani tunahitaji jumla ya bilioni 2 ili tuweze kutengeneza miundombinu ya maji Wananchi wa Singida wapate maji. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu ya uhakika kwa Mbunge huyu wa Ikungi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwanza namfahamu vizuri alikuwa Mkuu wa Wilaya, lakini nataka niwahakikishie wana-Singida Mashariki hili ni jembe wembe walitumie vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika kuhakikisha kwamba, tunatatua tatizo hili la maji tumeshafanya jitihada za uchimbaji. Nimuombe baada ya Bunge Saa saba tukutane tupange mikakati ya kwenda kutatua tatizo la maji kwa haraka kabisa. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Na mimi kama Spika naongeza, Wizara ya Maji Ikungi kule hakikisheni mambo ya maji matatizo yanaisha kabisa. (*Makofi*)

Swali linalofuata Mheshimiwa Esther Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini.

Na. 5

Ukosefu wa Maji Safi na Salama Jimbo la Bunda Mjini

MHE. ESTHER A. BULAYA aliuliza:-

Jimbo la Bunda Mjini limekuwa likikumbwa na adha ya ukosefu wa maji safi na salama na Serikali imekuwa

ikikwamisha mradi wa maji safi na salama Bunda kwa muda sasa kushindwa kutoa fedha za utekelezaji:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha, ili mkandarasi aweze kukamilisha mradi huo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJALIJIBU:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Amosa Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mji wa Bunda ni milongoni mwa maeneo ambayo yana shida kubwa ya maji. mahitaji ya maji kwa Wananchi wa Bunda mjini ni mita za ujazo 9,857 kwa siku wakati uzalishaji wa maji kwa sasa ni mita za ujazo 4,464 kwa siku. Hii inatokana na kutokukamilika kwa ujenzi wa miundombinu wa usambazaji maji baada ya mkandarasi kuondoka eneo la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mradi huo unakamilika na wananchi kuanza kunufaika na huduma ya maji, Serikali imechukua hatua kuainisha kazi zote ambazo hazijatekelezwa katika mradi huo, zinazogharimu kiasi cha shilingi milioni 375. Fedha hizo zinapelekwa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma, ili ziweze kusimamia utekelezaji wa mradi huo na kuukamilisha, hivyo kuanza kuhudumia Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini. Ni dhahiri kukamilika kwa mradi huu pamoja na ujenzi wa chujio jipya la maji kutasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua tatizo la maji katika mji wa Bunda.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Bulaya, nimekuona.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Spika wewe ni shahidi, huu mradi ni wa muda mrefu sana zaidi ya miaka 11. Miaka mitatu mizima tunazungumzia suala la chujio, si sawa kwa wananchi wa Bunda na Mkoa wa Mara. Naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, mbali na changamoto za wakandarasi kutokulipwa, mbali na changamoto za wakandarasi kuondoka *site*, Mamlaka ya Maji ya Mji wa Bunda kupitia vyanzo vyake vya ndani vimeanza kusambaza mitandao ya maji. Sasa nilitaka kujua Serikali mna mkakati gani wa kusaidia jitihada hizi za mamlaka ya maji Mji wa Bunda mbali na kwamba, haipati ruzuku Serikalini, kuendelea na zoezi la usambazaji wa miundombinu ya maji katika maeneo mbalimbali ikiwepo Manyamanyama, Bunda *Store*, Gerezani, Olimpas, Sazila; Serikali lini mtahakikisha hii mitandao ya maji yanafika kwenye maeneo hayo ambayo hakuna kabisa?

Mheshimiwa Spika, swalı langu la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri unajua Mamlaka ya Mji wa Bunda, Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda ni Mpya. Tumekuta kuna madeni ya umeme ambayo mwisho wa siku takribani milioni 603 hayo tumerithi. Mamlaka yangu ya Mji wa Bunda inalipa bili *current* bili inalipwa, lakini haya madeni yamerithiwa kupitia halmashauri iliyopita tangu Mzee wangu Wassira. Wizara mna mkakati gani kuhakikisha hli deni linalipwa, ili umeme usikatwe wananchi waweze kupata huduma ya maji maana wao ndio wanaoathirika na bili inalipwa?

SPIKA: Ahsante sana, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, cha kwanza nataka nikiri kwamba, moja ya changamoto kweli tuliyokuwanayo ilikuwa wakandarasi wababaishaji, lakini uanzishwaji wa RUWASA mmekwishatupa rungu sisi viongozi wa Wizara ya Maji, hatuna

sababu hata moja ya kulalamika. Tutachukua hatua kwa mkandarasi yejote ambaye atataka kutuchelewesha katika kukamilisha miradi yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kutokana na mradi ule Mheshimiwa Waziri amekwishatoa agizo kwamba, mradi ule sasa tutatekeleza kupitia wataalam wetu wa ndani katika kuhakikisha tunawapa uwezo Mamlaka ile ya Bunda kwamba, tutaoa milioni 375 na wataalam wetu wa ndani wataukamilisha mradi ule kwa haraka. Na kazi iliyobaki ni wataalam wetu wa mamlaka sasa kuwaunganishia wateja wao, ili waweze kupata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la ukatikaji wa umeme na madeni yaliyopo, hii ni *Grade C* mamlaka yao. Sisi kama Wizara yetu ya maji tumeona haja sasa ya wao kulipa kidogo na sisi tuweze kuwaongezea ili katika kuhakikisha tunakamilisha deni lile na wananchi wa Bunda waendelee kupata huduma ya maji. Pia natambua kwa Mheshimiwa Kangi Lugola kukamilika kwa mradi huu maeneo ya vijiji jirani kwa maana ya Buzingwe, Bulamba na Kabainja nao watapata huduma ya maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Esther Bulaya kukamilika kwa mradi huu utafanya maamuzi sahihi sasa ya kurudi nyumbani, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri umeelezea Jimbo la Bunda Mjini na Jimbo la Mwibara, lakini bado kwa Mheshimiwa Getere hujasema chochote. Mheshimiwa Mwita, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niwashukuru Wizara ya Maji kwa sasa kwa kweli tuseme ukweli kwamba, viongozi wote Mawaziri, Makatibu na watendaji wote sasa wako kazini, wanafanya kazi vizuri, niwashukuru sana. Katika Jimbo la Bunda wataalam walifanya tathmini ya kuchimba

visima vya maji ikaonekana kwamba, visima vinakauka, Wizara ikaja na mkakati wa kuchimba malambo zaidi ya malambo 16 ambayo ni matumizi ya maji, sasa kwa mwaka huu wamechagua kuchimba malambo matano. Nilitaka kuuliza tu Waziri, ni lini sasa haya malambo matano yatafanyiwa kazi? Ahsante.

SPIKA: Majibu mafupi kwa haraka, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kiukweli anafanya kazi kubwa sana. Jana tu tulikuwepo nae katika Wizara yetu ya maji na Katibu Mkuu na moja ya makubaliano ni katika kuhakikisha tunatia fedha kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa zaidi ya matano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nataka nikuhakikishie sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa Wananchi wako wa Bunda Vijijini kuweza kuchimbiwa mabwawa haya na waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, pia, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wa Mkoa wa Mara wanaotokana na Chama cha Mapinduzi kwa mshikamano wao na kuweza kupigana. Zaidi ya miradi Mgango, Kyabakari tumekwishesaini, lakini tunakwenda kutatua tatizo la maji Mugumu pamoja na Tarime. Ahsante sana.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Hawa Ghasia, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante ningependa kuuliza swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini tumechimbiwa visima 11 na kati ya visima hivyo, visima vitatu tayari Serikali imeridhia mchakato wa kutafuta mkandarasi uanze.

Je, ni lini Serikali itaridhia na visima vinane vilivyobaki navyo mchakato wa kutafuta mkandarasi uanze, ili huduma ya upatikanaji wa maji Jimbo la Mtwara Vijijiini iboreke?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, lakini la kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, mama yangu Hawa, kwa kazi kubwa anayofanya katika jimbo lake, lakini kikubwa nimuagize Mhandisi wa Mkoa kwa maana ya Meneja wa RUWASA katika kuhakikisha analifuatilia hili jambo na ahakikishe lianzu kwa haraka. Na sisi kama Wizara ya Maji tupo tayari kuwapa msaada, ili mradi huu uanze kuwaka kwa wakati.

SPIKA: Ahsante sana nakushukuru sana. Tunahamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linaulizwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale.

Na. 6

Barabara ya Kutoka Busisi Hadi Nyang'holongo

MHE. HUSSEIN N. AMAR aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, katika ziara yake Wilayani Nyang'hwale tarehe 11 Novemba, 2013 akiongozana na aliyekuwa Waziri wa ujenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Najaliwa alitoa ahadi kwa wananchi ya kujenga barabara ya kutoka Busisi – Busolwa – Nyijundu – Kharumwa, Bukwimba hadi Nyang'holongo kuelekea Kahama Mjini kwa kiwango cha lami pamoja na kuondoa tatizo la mawasiliano ya simu:-

(a) Je, ni lini ahadi hiyo ya viongozi wakuu wa nchi itatekelezwa?

(b) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hizo kwa kujenga minara ya mawasiliano ya simu ili maeneo ya Nyamtukuza, Kanegere, Nyugwa na maeneo mengine yaweze kusikika na kuchochea maendeleo ya nchi?

SPIKA: Majibu ya Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa, Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Busisi – Busolwa – Nyijundu – Kalumwa – Bukwimba – Nyang'hongo hadi Kahama yenye urefu wa kilometra 204.68 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) iliyoko katika Mikoa ya Mwanza kilometra 41, Mikoa wa Geita kilometra 68.68 na Mikoa wa Shinyanga kilometra 95.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya viongozi wa nchi ikiwemo ahadi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara tajwa itatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili iendelee kupidika majira yote ya mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, kufuatia ahadi iliyobolewa na Rais Awamu ya Nne na utekelezaji wa Sera ya Serikali, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliainisha uhitaji wa mawasiliano katika Wilaya ya Nyang'hwale yakiwemo ya maeneo ya yaliyoahidiwa ili kutambua maeneo yote yenye uhitaji wa mawasiliano kwa ajili ya ufikishaji wa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya tathmini hiyo, Serikali ilikuwa imejenga mnara wa mawasiliano katika Kata ya Shabaka mwaka 2013 yenye wakazi takribani 12,072 katika mradi uliotekelawa na Kampuni ya Vodacom.

Mheshimiwa Spika, baada ya uainishaji kukamilika na ukubwa wa uhitaji kubainika, Januari 2014, Serikali kuptitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilitangaza zabuni ya kufikia huduma za mawasiliano katika Kata za Busolwa, Kafita, Kakora, Nyijundu, Mwingiro, Nyabulanda na Nyugwa. Utekelezaji uliana Aprili, 2015 ambapo wakazi zaidi ya 68,544 ikiwemo Kata ya Nyugwa wamefikishiwa huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kutekeleza ahadi iliyotolewa kwa maeneo yaliyobaki ya Nyamtukuza, Kanegere na maeneo mengine illi yaweze kusikika na kuchochea maendeleo katika maeneo husika kadri ya upatikanaji wa fedha, hususan katika mwaka wa fedha 2019/2020.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kabla ya maswali kuna marekebisho kidogo katika maandishi aliyoandika hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, inasomeka barabara ya Busisi - Busolwa, Nyijundu - Kharumwa - Bukwimbwa - Nyang'holongo siyo Nyang'hongo.

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho hayo, napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa Serikali inakiri kutekeleza ahadi hizo za viongozi kwa kujengwa barabara ya lami kutoka Kahama hadi Busisi kuptitia Kharumwa pindi pesa zitakapopatikana. Swali la kwanza, kwa nini wakati Serikali ikitafuta fedha za

kutengeneza hizo kilomita nyingi tuisitengewe fedha za kujenga kilomita 3 Makao Makuu ya Wilaya Kharumwa ili kupunguza vumbi kutokana na msongamano mkubwa wa magari uliopo pale?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Naibu Waziri amesema wanaendelea na kupeleka mawasiliano katika kata alizozitaja lakini Kata ya Nyijundu kuna matatizo ya usikivu. Je, Vodacom wako tayari kwenda kufunga mnara huo ili wananchi wa maeneo yale waweze kutuma na kupokea fedha kupitia Mpesa?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tumezungumza mambo mengi sana kuhusu uboreshaji wa miundombinu katika Wilaya hii ya Nyang'hwale. Tulfanya *discussion* na Mheshimiwa Mbunge na anakumbuka nilitoa maelekezo upande wa wenzenetu wa *TANROADS* Mkao wa Geita kwamba tutazame Makao Makuu ya Mji ya Nyang'hwale. Kama tulivyokubaliana tutaanza na kilometra 2 pamoja na kuboresha mitaro iliyowekwa katika Mji wa Kharumwa, Makao Makuu ya Nyang'hwale. Kwa hiyo, nimtoe hofu tumejipanga kufanya Makao Makuu ya Nyang'hwale kukaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano, tunaendelea na hatua ya kuboresha mawasiliano nchi nzima. Nimsihi tu Mheshimiwa Mbunge baadaye tuonane ili tuangalie kwenye orodha maana kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tutapeleka mawasiliano katika vijiji 521 ambavyo viko kwenye kwenye hatua ya manunuzi inawezekana vijiji vyake vikawepo. Kwa hiyo, tuonane tu, ninayo orodha hapa,

nawakaribisha na Waheshimiwa Wabunge wengine ili tuone tumejipangaje kupeleka mawasiliano maeneo ambayo tumejipangia katika awamu hii ya nne. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Swali la nyongeza, nimekuona Mheshimiwa Aisharose Matembe.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Tatizo la miundombinu lipo pia katika Jimbo la Ikungi Mashariki katika barabara yetu ya Makiyungu - Misughaa. Changamoto hiyo imekuwa kubwa sana wakati wa masika. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mikoa ya Singida na Dodoma na kuharakisha shughuli za maendeleo katika maeneo hayo? Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aisharose Matembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Aisharose Matembe amekuwa mahiri sana kufuatilia barabara mbalimbali. Barabara hii anayoitaja Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya kilomita 461 ya barabara inayotoka Handeni - Kibirashi - Kijungu - Chemba - Singida. Kwa hiyo, nimuombwe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira kwani katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kuanza ujenzi wa barabara hii muhimu. Tukipata fedha eneo hili litapitiwa na mradi wa barabara ya lami inayotoka Handeni – Singida.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa Maige endelea.

Na. 7

Ujenzi wa Barabara ya Mwanza – Solwa – Bulige

MHE. AHMED A. SALUM aliuliza:-

Usanifu na upembuzi yakinifu wa barabara ya kutoka Mwanza – Solwa – Bulige kwa kiwango cha lami umekamilika:-

Je, ni lini mradi huu utaanza?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Solwa – Kahama yenye urefu wa kilometra 150 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) kuititia Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ilikamilika Desemba, 2017 kwa gharama ya shilingi milioni 798.8.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali sasa ni kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa na nchi jirani kwa barabara za lami zilizoainishwa kwenye Shoroba za Maendeleo (*Development Corridor*). Barabara nyingine ikiwemo ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Solwa – Kahama itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya

kuifanya matengenezo barabara hii ili ipitike majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi bilioni 1.6 zimetengwa.

SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige, swali la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu Chifu Kwandikwa kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Pamoja na majibu hayo mazuri nilikuwa naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara kubwa tatu zinazopita Jimbo la Msalala kwa maana ya barabara hii ya Solwa - Kahama kupitia Bulige; Busisi, Nyang'hwale - Kahama na Kahama - Geita, zote upembuzi yakini fu ulishakamillka. Bajeti ya mwaka huu mwezi Juni, tulipitisha fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kahama - Geita. Barabara hii imekuwa ni kero kubwa, nilitaka kujua na wananchi wafahamu ni hatua gani sasa imefikiwa ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kahama - Geita kuanzia pale Manzese - Segese - Bukoli - Geita?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri barabara ya Geita - Kahama ambayo inashuka mpaka Ushetu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyozungumza ukiangalia kwenye ukanda ule barabara hizi zote zinahusiana. Sisi kama Serikali tumejipanga kufanya barabara hizi ziwe kwenye mnyororo mzuri. Mheshimiwa Maige anafahamu hatua nzuri tuliyofikia ya ujenzi wa barabara hii kutoka Kahama kupitia maeneo aliyoyataja ya Bulige, Jimbo la Mheshimiwa Bukwimba kwenda mpaka

Geita Mjini. Tumejipanga na tupo kwenye hatua za mwisho kuanza ujenzi wa barabara hii muhimu. Hatua hii sasa itapunguza urefu wa barabara hii ambayo Mheshimiwa Nassor naye ameuliza hapa na nimejibu muda uliopita kwa maana itaunganisha barabara hiyo kwa maana ya kupita kwenye mji wa Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, hata barabara hiyo niliyojibu kwenye swalii la msingi inapita kwenye maeneo mengi, alijaribu kutaja maeneo machache. Kimsingi inagusa Jimbo la Misungwi, inapita kwenye eneo la Kwimba na inaunganisha pia Jimbo la Solwa, Msalala na Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa wananchi wa Kahama kwa ujumla na wananchi wa Mkoa wa Geita na Mwanza kwamba tumejipanga vizuri, tutaenda kwa awamu hivyo hivyo. Barabara hii kubwa itaanza lakini pia barabara hizi zingine tuko kwenye mpango wa kuzishughulikia. Tukionana baadaye ataangalia pia kwenye mpango mkakati wetu kama Wizara tumejipangaje hatua kwa hatua kukamilisha barabara zote hizi. Nampongeza sana kwa umahiri mkubwa katika kuwahudumia wananchi wa Msalala.

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, bado tunaendelea na Kipindi cha Maswali lakini naomba tusikilizane, nina matangazo mawili hivi.

La kwanza, nawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, Wenyeviti wetu wa Kamati muende hapa kwenye *lounge* ya Spika kwa kikao muhimu. Kwa hiyo, nawaomba popote pale mlipo Wajumbe wa Kamati ya Uongozi muende hapa nyuma kwa kikao muhimu ambacho kitaendelea hapo ili baada ya Maswali na Azimio moja kwa moja twende kwenye kikao chetu cha *briefing* ili pamoja na mambo mengine basi tuweze kutoa ripoti ambayo Kamati ya

Uongozi mtakuwa mmeidhinisha. Kwa hiyo, nawaomba sana Kamati ya Uongozi twende hapo kwa kikao kifupi tu, hakitakuwa kirefu.

Waheshimiwa Wabunge, la pili, niwatangazie kwamba hizi karatasi za pinki za maswali na *Order Paper* (Orodha ya Shughuli) kwa ujumla wake, hii ndiyo itakuwa karatasi ya mwisho kuingia Bungeni leo. Kuanzia kesho tutakutumia *Order Paper* hii kwenye mawasiliano yako ya kimtandao. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba kila mmoja a-*confirm* namba yake ya simu ya *WhatsApp* na *email address* hapa mezani. Sisi ndiyo Bunge pekee Afrika Mashariki ambalo bado tunaendekeza masuala ya makaratasi mengi, wenzetu wote ni *paperless*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tutaanza na hili jambo moja peke yake la hii *Order Paper* halafu tutaona kidogo kidogo kadri ambavyo tutaenda mpaka tutafika mahali ambapo dawati la Mheshimiwa Mbunge litakuwa safi. Kwa hiyo, tutaanza na hii kwa kutumia simu yako ya mkononi. Naomba kila mmoja atuhakikishie kuhusu namba yake ya simu ya *WhatsApp* na *email address* na mawasiliano mengine ya kimtandao ambayo anaona itakuwa bora Bunge tukatumia. Kuanzia kesho karatasi hii haitaingia hapa Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Badwel, Mbunge wa Bahi.

Na. 8

**Kukarabati Miundombinu Chakavu ya Skimu za
Umwagiliaji Bahi**

MHE. OMARY A. BADWEL aliuliza:-

Kwa sasa Dodoma ni Makao Makuu ya nchi yetu na kwa sababu hiyo idadi ya watu pamoja na mahitaji ya

huduma mbalimbali ikiwemo chakula vitaongezeka. Wilaya ya Bahi ambayo ni miongoni mwa Wilaya za Dodoma ina fursa muhimu za uzalishaji mchele kutokana na jiografia yake lakini inakwamishwa na miundombinu chakavu na isiyokamilika katika skimu zake za umwagiliaji wa zao la mpunga:-

Je, Serikali imejiandaa kuchukua hatua gani kutoa fedha za ukarabati na umaliziaji wa miradi hiyo ya umwagiliaji ili Wilaya ya Bahi ipate fursa ya uzalishaji mchele kwa wingi na kukidhi mahitaji ya chakula katika Mji wa Dodoma?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha na kukarabati miundombimu ya umwagiliaji chakavu iliyopo Wilaya ya Bahi, Serikali itafanya tathmini ya miradi hiyo kabla ya mwezi Desemba, 2019 na utekelezaji wake utahusisha wadau mbalimbali wa miradi ya umwagiliaji wakiwemo washirika wa maendeleo, wawekezaji binafsi na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa, kilimo cha umwagiliaji kinakuwa cha uhakika na kuongeza upatikanaji wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi pamoja na vyama vya wamwagiliaji wa maeneo hayo kuandaa maandiko kuomba mikopo kutoka taasisi za kifedha kama vile Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa lengo la kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya

umwagiliaji ili wananchi wa maeneo haya waweze kuwa na uhakika wa chakula cha kutosheleza kwenye maeneo yao.

SPIKA: Mheshimiwa Badwel, nimekuona swali la nyongeza.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, lakini pia nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza habari ya tathmini na mimi nashukuru kwa kuniahidi kwamba kabla ya Desemba tathimini hizo zitakuwa zimefanyika ili waweze kujua fedha ngapi zinahitajika ili kumalizla na kukarabati miradi hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa tayari tuna miradi ambayo fedha zake zinajulikana kwamba zikipatikana miradi hiyo inaweza kukamilika kwa mfano Mradi wa Umwagiliaji katika Kijiji cha Kongogo amba o umekuwa ni wa muda mrefu. Swali la kwanza, je, Serikali sasa iko tayari kupeleka fedha kabla ya hiyo tathmini kwa sababu tayari tathmini yake inajulikana ili mradi ule uweze kukamilika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amehusisha kwamba wako washirika mbalimbali amba o wanaweza kutusaidia katika suala zima la miradi yetu ya umwagiliaji na sisi Bahi tayari tunao wafadhili amba o wanatusaidia hususan Shirika la *L/C* ambalo nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa namna ambavyo wamesaidiana na kushirikiana vizuri na wananchi wa Bahi katika miradi hii ya umwagiliaji. Tayari wameshatuandikia andiko na michoro mizuri kabisa ya utengenezaji wa bwawa katika Kijiji cha Chikopelo lakini bado hatujapata fedha. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kupokea andiko hili kutoka wenzetu hawa Shirika la *L/C* ili kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri waweze kututafutia fedha katika mashirika haya mbalimbali ya wadau wetu? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kujua kama Serikali iko tayari kwa ajili ya kupeleka fedha kwa mradi huu wa skimu ya Kongogo ambayo ni ya muda mrefu. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Badwel kwa ufuatiliaji wa karibu sana na ushirikiano anaowapa watu wake wa Bahi. Sisi kama Serikali kwanza tuko tayari kwenda kupeleka fedha na ndiyo maana kwenye bajeti ya mwaka huu, mwaka 2019/2020 tumetenga zaidi ya shillingi millioni 217 kwa ajili ya kufanya tathmini ya miradi hiyo ukiwemo huu wa Kongogo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anataka kujua pia kama Serikali tuko tayari kuchukua andiko walilofadhiliwa na wadau hao wa maendeleo. Serikali iko tayari na sisi binafsi tulishaanza lakini baada ya Bunge hili kwisha tunaomba atupe hilo andiko tulifanyie kazi. Kama tulivyosema hela tulishatenga tutafanya kila liwezekanavyo ili na hili andiko tulitekeleze haraka iwezekanavyo.

SPIKA: Ahsante. Tuendelee na swali la Mheshimiwa Willy Qambalo, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Flatei kwa niaba yake.

Na. 9

Hitaji la Vyanzo Mbadala vya Umwagiliaji – Bonde la Eyasi

MHE. FLATEY G. MASSAY (K.n.y. MHE. QAMBALO W. QULWI) aliuliza:-

Wakulima wa Bonde la Eyasi wanategemea kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia chemchem za Qangded; na

kutokana na kupungua kwa kiasi cha maji katika vyanzo hivyo wakulima wengi wanashindwa kuzalisha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyanzo mbadala kama mabwawa na visima virefu ili kilimo katika bonde hilo kiwe endelevu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Jimbo la Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wakulima wa Bonde la Eyasi wanategemea kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia chemchemi za Qangded. Aidha, kutokana na kupungua kwa kiasi cha maji katika vyanzo hivyo pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali ikiwemo umwagiliaji, wakulima wanashindwa kuzalisha mazao ya kilimo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza vyanzo mbadala nya maji kama mabwawa na visima virefu, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu itafanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kubaini maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa na kuchimbwa visima virefu na hivyo kuongeza vyanzo nya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha upembuzi yakinifu, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu inashauriwa kutenga fedha zitokanazo na mapato ya ndani kama ilivyoelekezwa kuwa kila Halmashauri itenye asilimia 20 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Sekta ya Kilimo ikiwemo kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kutafuta vyanzo mbadala nya fedha ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Eyasi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria Na. 5 ya Umwagiliaji ya Mwaka 2013 tunatambua kuwa ushiriki wa sekta binafsi

katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kutafuta vyanzo vingine vyataga fedha ili kujenga mabwawa na visima virefu kwa kutumia utaratibu wa Jenga, Endesha na Kabidhi.

SPIKA: Mbunge wa Mbulu Vijijini, Mheshimiwa Flatey Massay, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. FLATEY G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri yanasema fedha hazipatikani na zitengwe kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri ya Karatu; na kwa sababu ukiangalia mapato ya Halmashauri hayana uwezo wa kujenga hata bwawa: Je, Serikali haionti sasa itumie namna mbadala kutoptana na hali hii ili kusaidia watu wa Bonde la Eyasi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Mbulu ziliikuwa Wilaya moja na Bonde la Eyasi ni sawasawa na Bonde la Bashai: Je, kuna mpango gani pia wa kusaidia Bonde la Bashai kulipatia fedha ili skimu hii ipate kuendelea?

SPIKA: Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mgumba, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, nashukuru. Swali la kwanza la Mheshimiwa Flatey Massay anasema kwamba Serikali ya Halmashauri ya Wilaya haina fedha ya kuweza kujenga hili bwawa wala miundombinu mingine mbadala wa vyanzo vyataga maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli, lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Serikali tutaendelea kutenga bajeti ile ya kiserikali kutoka Serikali Kuu kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, lakini kama tulivyoelekeza, naye

mwenyewe anajua. Hili Bonde la Eyasi kwenye kilimo tu cha vitunguu ndiyo linachangia mapato zaidi ya asilimia 33 ya Halmashauri hiyo ya Karatu, lakini haipeleki Halmashauri hiyo ya Karatu hata senti tano kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha vitunguu katika bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kama Serikali tumeelekeza watenge kwenye mapato yao ya ndani asilimia 20 ili kwenda kunenepesha ng'ombe yule wanayemkamua kwenye vitunguu ili waweze kukamua zaidi siku zijazo. Hatujasema kwanza hicho ni chanzo pekee cha kuendeleza huko, hapana. Hicho ni kimojawapo, ndio maana nimesema kwenye ile programu ya Jenga, Endesha na Kabidhi kuititia Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Benki ya Rasilimali pia wanaruhusiwa kwenda kuchukua mkopo. Tutaenda kujenga hiyo miundombinu baada ya kuiendesha halafu baadaye tutakabidhi baada ya mapato hayo kuisha. Pia tutaendelea kutenga kwenye bajeti kuititia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika swalii lake la pili, skimu hii iliyokuwa katika Wilaya ya Jimbo la Mbulu pia utaratibu utakuwa ni huo huo na ombi lake nimelipokea, ni vizuri alete sasa hilo andiko na tutatuma Tume ya Taifa ya Umwagiliaji waende huko wakafanye tathmini na kuangalia mahitaji, baadaye tutaingiza kwenye bajeti kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa skimu hiyo.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, Kilimanjaro.

Na. 10

Mpango wa Kuondoa Majiko ya Mafiga Matatu

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Afya za wanawake wengi vijijini zinaathiriwa na moshi wa kuni wanazopikia kwenye majiko ya mafiga matatu

ambayo yanatumia kuni nyingi na hivyo kuchochaea kasi ya ukataji miti:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa matumizi ya majiko ya mafiga matatu kote nchini?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuondoa majiko hayo kwenye shule zote za msingi na sekondari?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matumizi ya tungamotaka hususan kuni na mkaa kama chanzo cha nishati ya kupikia hapa nchini yanakadirwa kufikia asilimia 85. Matumizi ya tungamotaka ikiwemo mafiga matatu husababisha madhara ya kiafya kutokana na kuvuta hewa chafu inayotokana na kuni na mkaa kwa watumiaji pamoja na uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015, Serikali imekuwa ikihamasisha matumizi bora ya nishati ikiwemo teknolojia zinazopunguza gesi ya ukaa na matumizi makubwa ya kuni na mkaa kwa kutumia majiko banifu. Aidha, Serikali imekuwa ikihamasisha kuacha matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa katika kupikia gesi na mitungi (*Liquefied Petroleum Gas*), bayogesi, vifofali vya mabaki ya tundamotaka na majiko ya nishati juu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijiji (REA) kupitia Mfuko wa Nishati Vijiji pamoja na jukumu la kusambaza umeme vijiji inasaidia usambazaji wa teknolojia bora za kupikia hususan katika taasisi za Umma nchi nzima zikiwemo Shule, Magereza, Kambi za Wakimbizi na Zahanati.

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, nimekuona. Swali la nyongeza tafadhali.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu yao mazuri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; sasa hivi ni takribani miaka 53 toka tumepata uhuru na majiko haya yamekuwa yakinumika pamoja na athari zake. Je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha kampeni mahususi ya kutokomeza matumizi ya majiko ya mafiga matatu katika shule za sekondari, vyuo, *primary* na kote huko ili kuondoa athari hizo kama ilivyofanya kampeni ya kuboresha maabara na kuleta madawati kwa shule zote hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna makampuni binafsi ambayo yanasantambaza gesi hizo za kupikia (*liquid gas*) na pia kwenye mitungi midogo ambayo ni *affordable* ikiwemo *Mihan* na *Oryx*. Sasa Serikali iko tayari kushirikiana na makampuni hayo ili kupunguza athari za moshi unaowaumiza sana akina mama walioko vijijini na kwingineko na bado hawajapata elimu ya matumizi ya majiko hayo kwamba wanaumia ili waweze kupatiwa majiko hayo kwa bei nafuu? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa mama yangu Shally Raymond. Kwanza nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye eneo lake la Mkoa wa Kilimanjaro hususan kwa masuala ya wanawake na inadhihirisha kwa swali hili ambalo ameliuliza linalohusiana na masuala ya majiko ya mafiga matatu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza la nyongeza ameulizia kama Serikali ipo tayari kuanzisha kampeni ya

kuondokana na majiko haya hususan katika shule za sekondari na msingi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema kwenye jibu langu la msingi, tunatambua kwamba majiko haya ya mafiga matatu yana athari ya kimazingira na kiafya lakini kwa kuwa tumelitambua hilo, Serikali pia ina mpango wa usambazaji wa gesi asilia katika mikoa mbalimbali ambapo imeanza na mikoa saba ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Tanga, Dodoma na Morogoro lakini sambamba na hilo, Serikali pia imekuwa iki-support makampuni yanayohusiana na gesi ya *LPG*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa hatua hizi zinaendelea katika kuhakikisha kwamba kwanza gesi asilia inasambazwa katika maeneo mbalimbali ambayo ina bei nafuu, lakini pili kwa kushirikiana na makampuni yanayoingiza nchini *LPG* ili iweze kushusha bei, nina uhakika kwamba tutafikia hatua hiyo ya kupeleka nishati hii ambayo itatumika katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pia kuna makampuni mbalimbali ambayo yanashirikiana katika suala zima la usambazaji wa nishati jadidifu katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, nitoe wito tu katika makampuni hayo kuendelea kuiunga mkono Serikali ili iweze kufikia hatua ya kutangaza hiyo kampeni na ni jambo jema. Namwomba ye ye pamoja na Wabunge wote wa Viti Maalum, Wabunge wote na wananchi mbalimbali tuhamasishe utunzaji wa mazingira na utumiaji wa nishati mbadala hasa katika kupikia ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kweli yapo makampuni kama nane ambayo yanahusika na masuala ya uingizaji wa gesi ya *LPG ikiwemo Oil Gas Tanzania Ltd, Taifa Gas, Mount Meru Gas* lakini pamoja na hayo kuna *Lake Gas, Oilcom* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali imefanya? Tumeona kwa kuwa kiwango cha matumizi ya *LPG* kimeongezeka kutoka kwa mfano tani 90,000 mwaka 2016 mpaka tani 147,000 mwaka 2018. Kwa hiyo, ni wazi matumizi yameongezeka, kwa hiyo, tulichofanya, tunatafakari namna ambavyo gesi ya *LPG* inaweza ikaingizwa kwa mfumo wa uagizwaji wa pamoja. Tupo katika mazungumzo na wadau wa makampuni haya na taasisi mbalimbali ili kuwezesha kuweka mazingira wezeshi ambayo yataisaidia hata *EWURA* kuweza kupanga bei ambayo inaweza ikawasaidia watanzania kutumia gesi hii ili kulinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwa makampuni ambayo yanaagiza; kwanza nawapongeza kwa uwekezaji wanaofanya, waendelee kujenga miundombinu katika mikoa mbalimbali ili hii gesi ya *LPG* iweze kuwafikia Watanzania wote. Serikali itaendelea kuandaa mazingira wezeshi ili kuwezesha huduma hii ipatikane kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Athari ya moshi ni sawa na athari ya umeme unaopita juu ya nyumba za wananchi. Kuna mradi Mchikichini, Mtaa wa Ilala Kota eneo la Baghdad ambapo *TANESCO* walikubaliana na wananchi kuitisha umeme mkubwa sana juu ya nyumba zao lakini kwa kigezo cha kuwalipa fidia. Umeme umepita, umeme ulikuwa usiwashwe mpaka fidia ilipwe, lakini umeme umewashwa na fidia haijalipwa, watu wako chini ya umeme mkubwa na wanaathirika kiafya.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kujuu ni lini sasa Serikali au *TANESCO* itawalipa fidia wananchi hawa wa Mchikichini ambao wako hapo kwa zaidi ya miaka 50, huduma zote wanapata pale. Kuna kigezo kililetwa kuwa eneo lile ni

hatarishi. Wananchi hawa wamekaa hapa miaka 50 wana huduma za maji, umeme na wanalipa bili zote na kikubwa kabisa inapokuja uchaguzi maboksi ya kura yanapelekwa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na *TANESCO* wawafikirie wananchi hawa amba ni masikini, wawalipe fidia waondoke ili waondokane na athari ya kuathirika na umeme huu mkubwa katika nyumba zao. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hili muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira. Aah, Waziri wa Nishati, nimekuona. Mheshimiwa Dkt. Kalemani, tafadhalii.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Zungu kwa kuulizia na kufuatilia masuala ya fidia kwa wananchi Mchikichini. Ni kweli kabisa wananchi wa Mchikichini walipitiwa na umeme mkubwa katika Jiji la Dar es Salaam, Wilaya ya Ilala miaka sita ama saba iliyopita. Ni kweli katika eneo hilo bahati nzuri sana eneo hilo lilichukuliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Dar es Salaam lakini ni kweli wananchi hao wanatambulika na kwamba walikuwa wakidai fidia.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunafanya majadiliano ya kina sana na Manispaa ya Ilala ili kuhakikisha kwamba wananchi amba wanadai fidia ni wale ambao kweli waliathirika na fidia. Pili kwa sababu eneo hilo lilichukuliwa na Halmashauri ya Manispaa, tunafanya mazungumzo ili wananchi hao waendelee kupata haki yao kulingana na wanavyostahili.

Mheshimiwa Spika, la pili, nampongeza Mheshimiwa Zungu, wiki mbili zilizopita tumekaa na Mheshimiwa Zungu kupitia kwa Kamishna wetu wa Nishati na tumefanyia kazi kwa kina suala hili. Wananchi hao tunawasihi wawe watulivu wakati suala hili linafuatiliwa kati ya Wizara na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ili waweze kupatiwa haki yao ndani ya muda mfupi kadri inavyowezekana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunahamia Wizara ya Madini, swali la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara.

Na. 11

Wachimbaji Kuuza Madini ya Manganese Ghafi

MHE. ALEX R. GASHAZA aliuliza:-

Katika Jimbo la Ngara wapo wachimbaji wadogo wa madini ya Manganese katika Kata ya Murusagamba, Kijiji cha Magamba na tayari wamepata soko la madini hayo nje ya nchi ikiwemo India, Afrika Kusini na Uturuki:-

Je, Serikal iko tayari kutoa kibali kwa wachimbaji hao kuuza madini hayo yakiwa ghafi kutokana na kwamba hakuna mitambo ya uchenguaji hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imendelea kusimamia Sekta ya Madini kikamilifu kwa kuhakikisha shughuli za uchimbaji na biashara ya madini zinafanyika kwa kufuata sheria na taratibu za nchi ili rasilimali hiyo iweze kutoa mchango kwa Serikali kupitia malipo ya tozo stahiki za madini na pia itoe fursa ya ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Madini na kwa kuwa rasilimali hiyo siyo jadidifu (*non renewable*), mwaka 2017 ilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na kutunga sheria mpya ya Mali na Urithi wa Asili (*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017*) ambayo imerasimisha umiliki wa rasilimali madini kwa Taifa. Kupitia sheria hizo, Serikali imetoa zuio la usafirishaji wa madini ghafi pamoja na makinikia nje

ya nchi ili kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya uchenjuaji na uongezaji thamani wa madini nchini ambayo itatoa fursa ya ajira kwa Watanzaia na pia kutekeleza dhima ya Serikali ya kuwa na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto inayowakabili wachimbaji wadogo wa madini ya viwandani yakiwemo madini ya *manganese*, Serikali inakamilisha utaratibu unaotumika katika kipindi cha mpito hasa kwa wachimbaji wadogo waliokuwa wamezalisha madini yao na kulipia tozo zote za Serikali kabla ya zuio hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Gashaza, nyongeza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Spika, napongeza viongozi wote wa Wizara hii ya Madini, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na matokeo yake tunayaona.

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia kwamba tayari katika mchakato huu na katika ombi hili wameshatekeleza kwa sehemu kwa kuwapa kibali wachimbaji hawa kwa kuanza na tani 500, nashukuru na kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa lipo soko kubwa la madini haya ya *manganese* nje ya nchi; Uturuki, India, Afrika Kusini na tayari wachimbaji hawa wadogo wameunganishwa kwenye masoko hayo lakini uchimbaji wa madini hayo unahitaji mtaji mkubwa kwa maana mitambo pia ya kisasa, Serikali iko tayari kuwawezesha wachimbaji hawa wadogo wadogo ili waweze kupata mitambo kama *excavator*, *tipping trucks* ili waweze ku-meet uhitaji wa soko na kuongeza kipato kwa Serikali yetu na kwao binafsi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa vile miongoni mwa madini yanayopatikana katika Jimbo la Ngara ni pamoja na *Nickel*/na kwa muda mrefu tumekuwa tukisubiria kuona mradi huu wa Kabanga *Nickel*/unaanza ili kutoa ajira,

kuongeza kipato kwa wananchi wa Jimbo la Ngara na Watanzania kwa ujumla, ni lini mgodi huu utaanza ili kuweza kuleta tija kwa wananchi na kwa Taifa pia? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Nyongo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli soko la Manganese lipo ndani ya nchi na lipo nje ya nchi, na wachimbaji wadogo wamekutana sana na changamoto ya kuwa na upungufu wa mitaji kwa maana ya kununua vifaa vya uchimbaji, Serikali kupitia ule mradi wa *SMRP* ambaao ulikuwa unafadhiliwa na *World Bank* kupitia katika Wizara yetu ya Madini ilikuwa inatoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo, lakini ruzuku hizo hazikutumika vema inavyostahili ndipo tuliposimamisha utoaji wa ruzuku hizo na sasa hivi tunatoa elimu kwa wachimbaji, tunatoa taarifa za uchimbaji kwa maana ya *geological information* na hizi taarifa tunazipendekeza kuzipeleka, au tunazipedekeza na kuwashauri watu wa mabenki mbalimbali waweze kuzitambua taarifa hizi na kuweza kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo ili wachimbaji hao waweze kukopa na kununua vifaa mbalimbali ambavyo vinaweza vikatumika katika uchimbaji na kuongeza tija katika uchimbaji huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusiana na mgodi wa Kabanga *Nickel* ni kweli kabisa *nickel* hapo kipindi cha nyuma katika soko la dunia ilikuwa na bei ya chini sana ambapo uchimbaji wake ulikuwa hauna tija, kwa sababu bei ya *nickel* katika soko la Dunia ilikuwa chini ya dola 3.5 kwa *pawn* moja, lakini sasa hivi, bei ya *pawn* moja ya *nickel* imepanda kwenda hadi dola Sita katika soko la Dunia ambapo Wawekezaji sasa wameanza kuona kwamba wakiwekeza kwenye *nickel* itaweza kuwa na faida, katika ule mradi wa Kabanga moja ya leseni ambayo ilikuwa ni *retention license* ilifutwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mabadiliko ya sheria mwaka 2017 hapa tulipo ni kwamba ile *retention*

/license ipo na sasa hivi tunaifanyia mchakato wa kutafuta Mwekezaji ambaye tunaona yuko *serious* anaweza akawekeza, sasa hivi tuko tayari kutoa leseni hiyo kwa mtu yejote ambaye tunaona anaweza akafanya shughuli hiyo, mpaka sasa hivi tuna mchakato unaoendelea ndani ya Wizara yetu kuona namna ya kuweza kumpa Mwekezaji ambaye tunaona anaweza akawekeza kwa faida na mradi huo uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni wakati wowote watu wa Kabanga wataona mradi huo unaanza na ninapongeza Serikali kwa juhudzi zake za kupeleka umeme eneo hilo pamoja na miundombinu ya reli na barabara ambayo sasa itakuwa ni miundombinu muhimu katika utekelezaji wa mradi huu wa Kabanga *Nickel*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, nimemuona Mheshimiwa Joseph Mhagama tafadhalii kwa niaba yake.

Na. 12

Serikali na Watumishi wa UmmaKutumia Benki ya *TPB*

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI) aliuliza:-

TPB ni Benki ya Serikali na inamiliwa na Serikali kwa zaidi ya asilimia 90 lakini Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma yanatumia Benki nyingine katika huduma za Kibenki:-

(a) Je, ni nini msimamo wa Serikali katika kutumia huduma za Kibenki?

(b) Watumishi wa Serikali na Viongozi wote wa Serikali wanatakiwa kutumia *TTCL* katika huduma za mawasiliano ya simu. Je, kwa nini Watumishi na shughuli zote

za Serikali zisianze kutumia huduma za Kibenki kupitia Benki hiyo?

SPIKA: Majibu ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, blashara huria ya sekta ya fedha ilianza tangu mwaka 1991 mara baada ya kuitishwa kwa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991, pamoja na Kanuni zake. Kupitia sheria hiyo, Wawekezaji mbalimbali walifungua Benki binafsi hapa nchini na hivyo matumizi ya huduma na bidhaa za benki kuanza kuamuliwa na nguvu ya soko ikiwa ni pamoja na huduma na bidhaa za Benki za Serikali. Benki ya *TPB*, kama ilivyo kwa benki nyingine haina budi kujimarisha na kujitangaza yenyewe kwa lengo la kuuza bidhaa zake na hatimae kuvutia wateja zaidi ikiwa ni pamoja na Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi ya nguvu ya soko, Benki ya *TPB* imefanikiwa kujitangaza na kuimarisha huduma zake na hivyo kuvutia baadhi ya Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kutumia bidhaa zake. Miongoni mwa huduma za benki ya *TPB* zinazotumiwa na Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kwa sasa ni pamoja na akaunti ya muda maalumu, akaunti ya biashara, malipo kwa njia ya mtandao, kubadilisha fedha za kigeni, kukusanya mapato ya Serikali, kulipa mishahara ya watumishi, mikopo kwa watumishi, kulipa pensheni za wastaaafu pamoja na mikopo kwa wastaaafu wanaolipwa pensheni zao na Serikali pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo iliyopo ya uchumi huria, Serikali haina Mamlaka ya kumlazimisha Mtumishi au Taasisi ya Umma kutumia huduma za benki yoyote, ikiwemo benki ya *TPB*. Hivyo basi, ni jukumu la Benki ya *TPB* na benki nyingine kuboresha mifumo ya huduma na bidhaa zao ili kuvutia Watumishi wa Umma, pamoja na Taasisi za Umma kuanza au kuendelea kutumia huduma zao.

SPIKA: Mheshimiwa Mhagama swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niipongeze sana benki ya *TPB* kwa kufanya kazi vizuri na kuendele kujiboresha, nina maswali mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu ya kuanzisha benki zinazosimamiwa na Serikali popote duniani, sababu za kuanzisha Benki za Umma ni kwenda kua-*address* mapungufu ambayo sekta binafsi, Mabenki Binafsi yameshindwa kuyashughulikia. Miongoni mwa mapungufu hayo ambayo tunayo hapa Tanzania ni kwamba Wajasiriamali wengi wadogo wanashindwa kufanya biashara zao kwa sababu hawana mitaji, ni kwa namna gani Benki hii ya Posta inajitofautisha na benki zingine za kibiashara katika kusaidia Wajasiriamali wadogo nchini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili swali langu tumeona kwamba Benki ya Kilimo Tanzania haina matawi katika Mikoa mingi na Wilaya nyingi na Wakulima wanakosa mitaji ya biashara ni kwa namna gani sasa Serikali imejipanga kuitumia Benki ya Posta kama Tawi kama tawi la Benki ya Kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni jinsi gani *TPB* inajitofautisha katika kutoa huduma na benki nyingine za biashara, naomba kumpa taarifa kwamba Benki ya *TPB* kwanza ina Matawi katika Mikoa yote Tanzania na imekwenda katika Wilaya ambazo tunasema ni kama Wilaya za Vijiji ambako Mabenki mengi ya biashara hayajafika, kwa hiyo hilo ni jambo la kwanza walilolifanya kuwafikia wananchi wetu kule walipo. Pia, Benki ya *TPB* ina mfumo wa kukaa na Wajasiriamali kuwapa mafunzo na kuwapa mikopo ambayo ina riba nafuu ikishirikiana na Benki yetu ya Kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni jinsi gani inaweza kushirikiana naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu tayari Benki yetu ya Kilimo ilishafungua matawi yake kwenye Kanda, Kanda ya Mwanza na Kanda ya Kati, tayari wameanza kufanya kazi na sasa wanajiandaa kwenda kufungua Tawi lao Mkoani Mbeya ili kuhudumia Nyanda za Juu Kusini. Wakati tukiendelea kufungua matawi ya Benki yetu ya Kilimo, Benki ya Kilimo pamoja na Benki ya *TPB* wanashirikiana na kwa mwaka huu wa fedha peke yake wametoa mikopo zaidi ya bilioni 431 kwa wakulima wetu kwenye maeneo yale ambapo *TADB* haina matawi lakini *TPB* imeweza kufika.

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu sisi kama Wizara tunayosimamia sekta hii kuhakikisha kuwa wananchi wetu wakiwemo wajasiriamali wadogo pamoja na Wakulima wetu wanafikiwa na huduma hizi kupitia Benki hizi za Umma zinazoendeshwa kwa kodi zao.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo tafadhali uliza swali lako.

Na. 13

Kupata Soko la Uhakika kwa Zao la Chai

MHE. FREDY A. MWAKIBETE aliuliza:-

Wananchi wa Kata za Mpombo, Kandete, Isange na Luteba pamoja na Kata za Kabula, Lwanga na Lupata wanalima zao la chai kwa wingi lakini bei ya zao hilo ipo chini:-

Je, ni lini Serikali itatafuta soko la uhakika la zao la Chai ambalo litasababisha kupanda kwa bei kuliko bei ya sasa ya Shilingi 315 kwa kilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Innocent Bashungwa, tafadhalii.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Chai Tanzania ilitisha kikao cha wadau wa chai kilichofanyika Aprili, 2019 kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za wakulima ikiwa ni pamoja na kupanga bei elekezi ya chai kwa mwaka 2019 kwa kuwashirikisha wadau wote. Mkutano huo wa Wadau wa zao la chai ulifanyika tarehe 3 Aprili, mwaka 2019 Mufindi Mkoani Iringa na Wajumbe walipitisha bei elekezi ya majani mabichi ya chai kwa mwaka 2019 kuwa ni shilingi 315 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali kutafuta masoko ya mazao ya kilimo nchini ni jukumu endelevu. Kwa upande wa zao la chai, jitihada zinafanyika ili kuhakikisha kuwa chai inayozalishwa inauzwa hapa nchini bila kuwalazimu Wakulima kusafirisha chai yao kwenda kwenye

mnada wa Mombasa. Katika kutekeleza hilo, Serikali inakamilisha mkakati wa kuanzisha soko la chai Tanzania kwa kuanzisha mnada wa Kimataifa wa Chai Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza uanzishwaji wa mnada wa chai nchini Tanzania kikosi kazi kiliundwa ambacho kinajumuisha Bodi ya Chai (*TBT*), Soko la Bidhaa Tanzania (*TMX*), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi wa Ghala, Chama cha Wakulima wa Chai Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (*TANTRADE*) pamoja na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wadogo wa Chai Tanzania yaani (*TSHTDA*). Maandalizi ya mnada huo yanatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2019 ili tuwe na mnada wetu utakaosaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa chai nje ya nchi na faldha inayopatikana iongeze bei ya mkulima.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Fredy swali la nyongeza tafadhali.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nipongeze Serikali kwa juhudhi pekee ya kuinua bei ya zao la chai kutoka 241 kwa kilo ya majani mabichi chai mpaka kufikia 315, na nimpongeze kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Rais kwa kutembelea Jimbo hili la Busokelo na *concern* yetu ya zao la chai tuliwaambia na kuunda Tume kwa ajili ya kushughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mwakaleli tuna Kiwanda cha Chai ambacho kimekuwa kikizalisha chai lakini kwa msimu, kuanzia mwezi wa Disemba mpaka Juni kila mwaka na hivyo miezi Sita mingine huwa hakifanyi kazi; Je, Serikali ina mpango gani mkakati wa kukifanya kiwanda hiki cha chai cha Bonde la Mwakaleli kiweze kufanya kazi mwaka mzima badala ya sasa tunaki- *underutilize*. (*Makofii*)

Swali la pili, hivi sasa katika Jimbo langu la Busokelo tunalima viazi mviringo na ni wakati wa msimu wa mavuno lakini bei yake ipo chini sana, kiasi kwamba hata wanunuzi wa viazi hivi wanawaibia zaidi wakulima wana-*collude* kwa kushirikiana na yale makampuni yanayotengeneza mifuko kwa kufanya kitu kinachoitwa lumbesa. Kwa mfano, mfuko mmoja ambao una debe tano wao wanafanya debe sita na nusu na wananchi hawa wanakuwa wamekopa wamenunua pembejeo, wamelima kwa shida, lakini bei zao ziko chini na kiasi hiki kinafanya mkulima akate tamaa kabisa kuendelea kulima zao hili la viazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inatoa tamko gani wewe ukiwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kuja *site* ili uone namna mateso ya wananchi wangu wa Bonde la Mwakaleli, Busokelo pamoja na Wilaya nzima ya Rungwe hadi Uyole - Mbeya kwamba wanahitaji masoko ya uhakika katika zao hili la viazi. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara majibu ya maswali hayo muhimu tafadhalii.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakibete Mbunge wa Busekelo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mwakibete kwa pongezi kwa Serikali kuongezeka kwa bei ya chai kutoka shilingi 241mpaka shilingi 315 lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Mwakibete kwa kweli anawapambania wananchi wa Busekelo tunakupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la Mheshimiwa Fredy Mwakibete Mbunge wa Busekelo ni kuhusu Kiwanda cha Chai kuzalisha miezi Sita peke yake na yeye angetamani pamoja na wananchi wa Busekelo kuona kiwanda hiki kinazalisha kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoomba nitatenga muda niweze kwenda nae Jimboni Busekelo tutembelee Kiwanda hiko tuangalie changamoto zilizopo na kuona ni nini Serikali inahitaji kufanya na upande wa Mwekezaji wanahitaji kufanya nini ili kuhakikisha kiwanda hiki kinazalisha kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Mwakibete angependa kuujua nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wananchi wake wa Busekelo tunawapatia soko la uhakika la viazi mviringo.

Mheshimiwa Spika, katika ziara ambayo nitaifanya tutahakikisha tunatoka na mkakati wa kuwapatia masoko ya uhakika wa viazi mviringo tunaujadili na pale inapowezekana tutawaunganisha wakulima hawa kwenye masoko ya viazi mviringo. Suala la lumbesa, halitasubiri ziara Mheshimiwa Mbunge baada ya maswali tutakaa pamoja tuangalie namna ya kushughulikia jambo hili, haliwezi kusubiri ziara, tutafuta namna ya kuliratibu vizuri ili wananchi wako wasiendelee kupunjwa kuititia mfumo wa lumbesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Swalii linalofuata ni swalii la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, uliza swalii lako tafadhali.

Na. 14

Ukosefu wa Viwanda na Masoko

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Makambako ili kupisha ujenzi wa soko la Kimataifa?

SPIKA: Bado tuko Viwanda na Biashara, majibu ya swalii hilo la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara tafadhali majibu.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Neema William Mgaya Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa soko la Makambako uliana baada ya Serikali kuona umuhimu wa kujenga masoko ya kimkakati (*Strategic Markets*) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ya Wakulima. Soko hilo lilibuniwa, ili kufanikisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa mazao ya kilimo hususan nafaka za mahindi na mchele ambazo huzalishwa kwa wingi katika Mikoa ya Njombe, Ruvuma na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwaka 2018 Serikali ililipa kiasi cha shilingi 3,026,341,089.58 ikiwa ni fidia kwa wananchi 209 wa Makambako ili kupisha ujenzi wa soko hilo. Aidha, wakati wa ulipaji fidia, walijitokeza wananchi 15 ambaao wakati wa uhakiki wa mwisho hawakupatikana na wananchi 20 ambaao hawakuwepo kwenye daftari wala taarifa ya uhakiki. Kwa muktadha huo, Serikali imeamua kufanya tathmini tena kwa wananchi ambaao hawajalipwa fidia zao ili waweze kulipwa kama wanastahili.

Mheshimiwa Spika, ninaupongeza uongozi wa Mkoa wa Njombe na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa huo kwa ushirikiano walioutoa katika zoezi zima la ulipaji fidia kwa wananchi waliopisha mradi wa ujenzi wa soko la Kimataifa la Makambako. Zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi wote litakapokamilika litawezesha mradi husika kutekelezwa bila kuwa na vikwazo.

SPIKA: Mheshimiwa Neema tafadhali.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua lini Serikali itamaliza kufanya tathmini hiyo ya pili na kuweza kulipa fidia kwa wananchi hawa wa Halmashauri ya Makambako ambao walikubali kabisa kupisha ujenzi wa soko la Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili, Wizara ya Viwanda na Biashara mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba ndani ya Mkoa wa Njombe na Tanzania kwa ujumla kunakuwa na viwanda vingi vidogo vidogo vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ili wanapoenda kuuza kwenye viwanda vikubwa na kwenye soko la Kimataifa tarajiwa wananchi hawa waweze kupata mapato zaidi na kuinua hali zao za kiuchumi, vilevile ili tuweze kufikia azma ya uchumi wa kati. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa tafadhalii.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge Neema Mgaya kwa namna anavyofuatilia changamoto za wananchi wa Mkoa wa Njombe, nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza la Mheshimiwa Mgaya ni kwamba lini tathimini itakamilika. Kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kuhakikisha tunawasaidia wakulima wetu kupata masoko ya uhakika, jambo hili tunalichukulia kwa uzito na tathmini, tutahakikisha inafanyika haraka iwezekanavyoo na kwa vile kuititia Wabunge, wananchi watatupa ushirikiano katika kukamilisha suala la fidia, basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tathmini itakamilika haraka iwezekanavyo, ili kuititia soko la kimataifa la Makambako, wakulima wanaotoka kwenye Nyanda za Juu Kusini waweze kuzalisha kwa wingi na kupata masoko ya uhakika kuititia soko la kimataifa la Makambako.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Mgaya angependa kujua nini mkakati wa Wizara yetu katika

kuhakikisha tunaongeza viwanda vidogovidogo ili kuchakata mazao ya wakulima. Nimehakikishi Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tayari ina mikakati mizuri, *bilaterally* kwa kuandaa makongamano mbalimbali nchini, ambapo wafanyabiashara kutoka nchi za SADC, wafanyabishara kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanakuja hapa Tanzania kukutana na wafanyabiashara na wenye viwanda hapa nchini, lengo hilo na mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kupitia *forum* hizi tunavutia uwekezaji lakini tunasaidia wafanyabiashara na wenye viwanda nchini ku-*network* na wenzao ambao wanatafuta fursa za kuwekeza hapa nchini na kwa vile utekelezaji wa *blue print* unakwenda vizuri, basi nina imani kabisha mikakati hii itaweza kusaidia kuchochea ujenzi wa viwnada nchini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana, swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Halima Bulembo!

Na. 15

Mikopo ya Chuo Kikuu Kutolewa kwa Ubaguzi

MHE. HALIMA A. BULEMBO aliuliza:-

Je, kwa nini mikopo ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu imekuwa ikitolewa kwa ubaguzi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Tate Olenasha! Majibu Mheshimiwa Laigwanan!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo Sura 178 ya sheria zetu, ambayo inabainisha sifa za msingi ambazo ni; awe ni mtanzania aliyedahiliwa katika masomo ya shahada katika taasisi inayotambuliwa na Serikali; na asiwe na vyanzo vingine vinavyoghamramia masomo yake. Kwa mwanafunzi anayeendelea na masomo, awe amefaulu kuendelea na masomo katika mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, bodi ina mamlaka ya kuweka utaratibu wa kubaini wahitaji, hivyo, bodi huandaa mwongozo unaoweka masharti kwa waombaji pamoja na maelekezo juu ya mambo muhimu ya kuzingatiwa kwa waombaji ambao ni yatima, wenyewe ulemavu au wenyewe wazazi wenyewe ulemavu na wale ambao masomo yao ya sekondari au stashahada, yalfadhiliwa. Maelekezo hayo ni pamoja na kuambatanisha uthibitisho wa hali zao.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubaguzi wowote katika utoaji wa mikopo, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu hutolewa kwa watanzania wote wenyewe uhitaji na walioomba mikopo hiyo kwa kuzingatia sheria, taratibu na vigezo vilivyowekwa. Hivyo, ni vyema waombaji kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na bodi wakati wa uombaji wa mikopo, ikiwa ni pamoja na kujaza taarifa zao kwa usahihi na kuambatanisha nyaraka zote muhimu.

SPIKA: Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, wanafunzi wengi waliokuwa wanasoma shule binafsi wamekuwa wakinyimwa mikopo ya elimu ya juu kwa kigezo kuwa wazazi wao wana uwezo wa kuwalipia. Je, ni kwa nini sasa Serikali isifute kigezo hicho kwa sababu si wanafunzi wote wanaosoma binafsi wana uwezo, lakini wengine wamekuwa wakienda binafsi kwa kukosa nafasi katika shule za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Bulembo ni kati ya Wabunge wanaowakilisha vijana Bungeni na hakika na hili sidhani kama ni la mjadala, amejitahidi sana katika miaka hii muhimu kufanya kazi yake vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nina hakika vijana wenyewe wanamfuatilia na hata anapouliza swali hili sasa la leo, ni katika jitihada hizo za kuwakilisha vijana katika Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sheria yetu inayotuongoza kwenye mikopo haibagui watoto wanaosoma kwenye shule binafsi. Sheria inataka tu tutumle vigezo vile vya kuangalia uwezo wa mtu kujillipia masomo ya chuo kikuu. Kwa hiyo, kinachofanyika ni kwamba, waombaji wote tunawafanyia kitu kinaitwa *minutes testing*, wanajaza fomu, tunangalia taarifa na kuangalia kama wanaweza wakajifadhili. Kwa hiyo, mtu anaweza akawa amesoma kwenye shule binafsi, lakini kumbe amefadhiliwa, tunachoomba, kama mtu amefadhiliwa, alete ushahidi, alete kiambatisho wakati anajaza fomu.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu, kuna wanafunzi 500 ambao wamesoma shule binafsi, wengine wamesoma mpaka *Feza School*, lakini kwa sababu wameleta uthibitisho wa kwamba wamesomesha na wazazi wao hawana uwezo, tunawasomesha. Kwa hiyo, naomba niendelee kutoa rai na ufahamu kwamba, kusoma kwenye shule binafsi siyo kigezo cha kukosa mkopo! Tunaaangalia uwezo, inawezekana mtu amesoma lakini kafadialiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile ifahamike kwamba, tuna rasilimali kidogo na tuna wahitaji wengi, ndiyo maana, kama tukipata fursa ya kutoa mikopo, tutatoa kwanza kwa wale ambao hali zao ni mbaya zaidi, kabla hatujatoa kwa wengine kwa sababu tunataka tulete

ulinganisho katika elimu. Tunafanya kitu kinachoitwa *equity*, kwa hiyo, hakuna upendeleo, ni sheria ambayo imetungwa na Bunge hili, ndiyo inatuelekeza.

Mheshimiwa Spika, na katika miaka hii tumefanikiwa kuendelea kuongeza wigo wa wanafunzi wengi kupata mikopo na ndiyo maana mwaka huu tumeweza kuongeza kutoka wanafunzi 41,000 wa mwaka wa kwanza, hadi kufikia wanafunzi 45,000. Nina hakika tutaendelea kuboresha taratibu hizo za kutoa mikopo na ikiwezekana huko mbele ya safari, kadri uwezo utakavyoruhusi, inawezekana hata kila mtu yejote anayetaka mkopo akapata. Isipokuwa tunapenda kuendelea kusisitiza kwamba ule ni mkopo. Kwa hiyo, kama mzazi ana uwezo wa kumsomesha mwanaye, asitafute mikopo kwa sababu baadaye atawajibika kulipa.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ili uweze kwenda chuo kikuu ni lazima uwe na ufaulu unaostahili na ufaulu huu unategemea jinsi ambavyo wanafunzi wametengenezwa, wanafunzi wamejengwa kuanzia ngazi ya Msingi hatimaye Sekondari, *A-Level* na *O-Level*.

Mheshimiwa Spika, hali ya ufaulu ndani ya Mkoa wa Lindi ni mbaya, ni mbaya! Mkoa wa Lindi bila kuzungusha, umekuwa wa mwisho katika ufaulu. Kwa misingi hii, kuwa wa mwisho si tatizo, unaweza ukawa wa mwisho katika mazingira ya kufanya vizuri, lakini unaweza kuwa wa mwisho katika mazingira ya kufanya vibaya.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa, Lindi tumekuwa wa mwisho katika mazingira ya kufanya vibaya, Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia changamoto zilizojitokeza ndani wa Mkoa wa Lindi mpaka kuwa wa mwisho? Na hii itapelekea kwamba kama Mheshimiwa Waziri husika akija na kuangalia nini changamoto zinazokabili Mkoa wa Lindi

kuwa wa mwisho? Naomba Mheshimiwa Waziri, atengeneze ziara ili aje atambue changamoto zinazokabili Mkoa wa Lindi, pamoja wana Lindi wenyewe wameshakaa vikao vya mkakati kuangalia changamoto hizo. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Lindi ya mwisho unasemaje Mheshimiwa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze mama yetu Mama Salma Kikwete, hakika amekuwa mama mpambanaji sana kuhakikisha elimu inasonga mbele kwa wato wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nilichukue jambo hili na ni kwell, Lindi imekuwa haifanyi vizuri na ndiyo maana hapa kipindi cha katikati, Ofisi ya Rais TAMISEMI kuona hivyo, niliweza kumtuma Naibu wangu Waziri Waitara alikwenda Mkoani Lindi kwa ajili ya kutembelea mionganini mwa shule mbalimbali na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo lengo letu kubwa ni kuboresha shule zile kwanza mazingira yawe rafiki zaidi na ndiyo maana maombi ambayo Mama Kikwete naye aliyomba hasa katika shule mfano kama ile Lindi Sekondari. Ndiyo maana hata katika kipindi cha sasa hivi hapa, tutakwenda kuifanya ukarabati shule yote ya Lindi Sekondari, lakini siyo Lindi Sekondari, isipokuwa kuzipitia shule za Lindi kuziweka katika mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwenyewe nitafanya ziara maalumu Mkoani Lindi kwa ajili ya kuhakikisha jinsi gani tunafanya kuufanya mkoa huu sasa uinuke kielimu na ndiyo maana hata katika mgao wa walimu, kipaumbele chetu sasa hivi tunaona kwamba jinsi gani hata badaye tupeleke walimu wa kutosha na hata uhamisho wa walimu katika Mkoa wa Lindi hivi sasa tumesimamisha kaika mkoa ule kwa lengo kubwa kwamba mkoa huu tuweze kuu-*promote* uwe katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu! Lindi ya mwisho, mikakati ya wizara.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa mama yangu Salma Kikwete. Kwanza nimpongeze sana mama Salma Kikwete kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika kuhakikisha kwamba elimu inasonga mbele na hasa kwa mtoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, na kuhusiana na swalı lake, pamoja na majibu mazuri ambayo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI ameyazungumzia kuangalia miundombinu, nami nimuahidi Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kama Wizara ya Elimu, ambayo kazi yetu ni kuweka Sera ya Elimu na kuhakikisha kwamba viwango vya elimu vinafikiwa, tutafanya ukaguzi maalum katika Shule za Mkoa wa Lindi, ili tuweze kubaini changamoto ambazo zinapatikana na tuweze kuchukua hatua mahususi kuhakikisha kwamba Mkoa wa Lindi unainuka katika ufaulu kwa wanafunzi ambao wanasoma katika shule za sekondari na shule za msingi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Elimu! Mheshimiwa Suzan, swalı la mwisho la nyongeza.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu ya Serikali, kilio kikubwa cha wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu ni pamoja na tozo ya asilimia moja kwa ajili ya *administrative costs* za bodi. Nilitaka kujua, Serikali haioni kwamba huku ni kuwaibia wanafunzi? Kwa sababu tunajua tuna bodi nyingi ambazo hazitegemei makato ama ya watumishi au ya wafanyakazi wake, ni kwa nini Bodи ya Mikopo unawatoza wanufaika asilimia moja kwa ajili ya *administrative costs* za bodi!

SPIKA: Majibu ya swalı hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Mheshimiwa Olenasha, tafadhalii!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali inatoza tozo ya asilimia moja kama *management costs* kwa ajili ya mkopo unaotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu, lakini ifahamike kwamba, kazi ya kuweza kufuatilia na kutoa mikopo ile ina gharama kubwa na ni kawaida katika utoaji wa mikopo, kwamba mkopo ule vilevile uweze kugharamia uendeshaji wake, vinginevyo inahitaji utafute fedha za ziada ili kuendesha ule mkopo.

Mheshimiwa Spika, asilimia moja anayosema Mheshimiwa Mbunge, inatozwa mara moja, haitozwi kwa mwaka. Kwa hiyo, ni *one off payment* na ukiangalia, ukilinganisha sisi tunachotoza na nchi zingine, sisi tunatoza asilimia ndogo sana, hata kwenye tozo zingine kwa ujumla wake. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba utoaji wa mkopo unafanya kwa ufafaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, na nimhakikishie tu kwamba, asilimia hiyo moja, imetuwezesha katika hii miaka minne kuongeza marejesho ya mikopo kutoka shilingi bilioni 23 toka mwaka 2015/2016 mpaka sasa kufikia bilioni 183 mwaka huu. Ile fedha inatusaidia kufuatilia kwa sababu watu ambao hawataki kutoa ni wengi, ina gharama. Kwa hiyo, naomba ajue tu kwamba lengo letu siyo kuwaumiza wanafunzi wala wazazi lakini ni kuhakikisha kwamba mikopo ile inarejeshwa na inatolewa kwa utaratibu ambao ni mzuri na yeye mwenyewe ni shahidi, yeye mwenyewe ameshatusifu mara nydingi kwamba tumefanikiwa sana kwenye elimu ya mikopo ya elimu ya juu.

SPIKA: Mheshimiwa Khadija Nassir ulisimama sana, malizia swalii la mwisho kabisa la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ukosefu wa Ofisi za Bodi ya Mikopo kwa upande wa Zanzibar umekuwa ukileta usumbufo mkubwa sana kwa wazazi na wanafunzi kusafiri kuja Dar es Salaam kwa ajili ya huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia hali duni ya wazazi, ni lini Serikali itasogeza huduma hizo kwa upande wa Zanzibar. Ahsante.

SPIKA: Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na changamoto hiyo ya ofisi kutoka Zanzibar, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tayari kuna jitihada za kuhakikisha kwamba ofisi inakuwepo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na ofisi kutokuwepo, bodi ya mikopo imeendelea kurahisisha namna ya kuomba mikopo na kurejesha, kiasi kwamba unaweza ukafanya maombi na kurejesha popote ulipo kwa sababu siku hizi kuna teknolojia, lakini naomba vilevile nimhakikishie kwamba bado kuna jitihada za kuhakikisha Zanzibar nayo inakuwa na ofisi.

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Sasa naomba niende kwa upande wa wageni, Mbunge aliyeapishwa leo hapa Bungeni Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, amekuja na wageni 244 waliomsindikiza kutoka Singida. (*Makofi*)

Katika wageni hao wameongozwa na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. (*Makofi/Vigelegele*)

Kwanza wale wageni wote toka Singida naomba msimame pale mlipo, wote mliokuja kutoka Singida. Safi kabisa! (*Makofi*)

Eee! wale wanaosomasoma mitandao na kujidanganyadanganya, ujumbe ndiyo huo kutoka Singida. (*Makofi/Kicheko*)

Singida imeongea hapahaha Bungeni, wote mnaona na mnashuhudia. Naomba mkae, niwatambulisse baadhi

kama nilivyosema Diana Chilolo anaongoza, lakini pia wako Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM ya Wilaya ya Ikungi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mika Likapakapa, Kamati ya Siasa ya Wilaya! Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wako Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, yuko Mkuu wa Wilaya ya Ikunge, Ndugu Edward Mpogolo, karibu sana, yuko Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Ndugu Rahabu Mwagisa, karibu, yuko Mkuu wa Wilaya ya Singida Pascas Mlagiri. Kuna wakuu wa wilaya watakuwa wamechelewa mahali. (*Makofi/Vigelegele*)

Pia iko familia ya Mheshimiwa Mtaturu, akiwemo Mama Mzazi wa Mheshimiwa, Amina Mohamed Mtaturu ahsante mama, ahsante sana. Yuko shemeji yetu, mke wa Mheshimila, Mwahija Mbwana Mtaturu, karibu sana Mwahija, wako watoto wa Mheshimiwa Mtaturu, yuko Jumanne Miraji, yuko Sabreena, yuko Salha karibuni sana watoto wazuri na ameambatana na wapiga kura kama walivyokuwa wamesimama kwa wingi kabisa, kabisa karibuni sana ndugu zangu wote toka Singida Mashariki. (*Makofi*)

Wageni wengine walikosa nafasi kwa hiyo, wako *basement*, tunawakaribisheni sana wote mliokuja na mimi ndugu zangu wa Singida Mashariki natoka hukohuko pia, maana nilikulia na kusoma Shule ya Msingi Marae, kule kule karibu na Mahambe, karibu na Ikungi hapo hapo, tuliwahi kucheza mpira sana enzi hizo. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ana wageni 38 ambao ni Wanakwaya wa Kanisa la TAG, Mkoa wa Dodoma. Nafikiri pia wamekosa nafasi wako *basement*. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Pascal Haonga, Ndugu Stela Leonard Mbaga. (*Makofi*)

Wengine ni wageni 33 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi. (*Makofi*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni wapiga kura wake na Watendaji wa Kata kutoka Jimbo la Nyamagana wakiwemo Ndugu Benedict Kabadi. (*Makof*)

Wageni wote tunawakaribisha sana hapa Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wakristo kwamba kutakuwa na ibada *Chapel* ya Bunge leo tarehe 3 Septemba, 2019, saa saba mchana. Mtumishi wa Mungu Mheshimiwa Innocent Bilakwate atahudumu katika ibada hiyo. Wale mliokuwa hamjui Mheshimiwa Innocent Bilakwate naye ni mpakwa mafuta wa bwana, sasa wengine msiwe mnamsogelea, msimpitie karibu. (*Makof/Vigelegele*)

Pia mzazi mwenzetu Mheshimiwa Livingstone Lusinde atakuwa na shughuli ya kuagwa kwa binti yetu Neema (mtoto wake) tarehe 6 Septemba, 2019 katika ukumbi wa Kilimani. Waheshimiwa Wabunge tunatarajiwa kwa wingi kabisa jioni ya tarehe 6, tujitokeze pale, tumsindikize binti yetu. Mheshimiwa Lusinde amekua sasa, kwa hiyo, wale waliozoea kumtania muache na karibu anaozesha, ahsante sana. (*Makof*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo ni mmoja tu, nimekuona Mheshimiwa Susan.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

SPIKA: Ooh na Mheshimiwa Lubeleje, tunaanza na Mheshimiwa Susan. (*Kicheko*)

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wakati ukitoa maelekezo kuhusiana na utumiaji wa *Order Paper* umesema kwamba leo ni mwisho na kesho tutaanza kutumia mtandao au simu zetu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka siku za nyuma tuliwahi kuambiwa Wabunge wote tutapewa *iPads* au *Tablets* lakini mpaka leo hatujapewa. Ikumbukwe kwamba kuna baadhi ya Wabunge ambao hawana simu za *android* lakini hata kama wanazo *sometimes* humu ndani kunakuwa hakuna mawasiliano mazuri na kwa maana hiyo tunahitaji *WiFi*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kama zoezi hili linaisha leo maana yake ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi au baadhi hawatakuwa na *access*ya mtandao huu kwa sababu ya matatizo mbalimbali ama watakuwa hawana *bundles* na hata kama wanakuwa na *bundles* saa nyingine kuna matatizo makubwa sana kwenye *line* zingine. Naomba mwongozo wako kwamba watu waendelee ili kuwapa muda Waheshimiwa Wabunge waweze kununua simu za *android*. Vilevile tunaomba tuwe na uhakika kwamba humu ndani kutakuwa na *WiFi* ili tuweze ku-*access* simu zetu kwa uhakika zaidi. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba mwongozo kuhusu swali Na.4, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji imekuwa ni tatizo katika nchi hii, inachukua miaka mingi haikamiliki, inachukua miaka minne mpaka mitano na fedha ni za hapa hapa ndani hazitoki nje. Tunaomba Waziri wa Maji atoe kauli hapa Bungeni, kwa nini miradi inachukua miaka mitano, sita haikamiliki?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante sana. Nikianza na Mheshimiwa Lubeleje, Serikali imesikia italitazama jambo hilo na kwa wakati wake watatushauri namna gani ya kwenda mbele kuhusu jambo hilo. Ni kero ambayo Wabunge wote kwa kweli inatugusa sana hasa tunapoelekea kwenye kimbembe maana bado mikutano mitatu tu, halafu sasa inakuwa tena miradi bado ehee. Kwa hiyo, Serikali baadaye watatushauri namna gani ya kuendana na jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu lile la mwanzo la matumizi ya mtandao, hizi changamoto za WiFi mtuachie lakini niseme kwa uhakika lazima tuanze mahali tutacheckwa mpaka lini? Hivi sasa mnajua Mabunge ya Afrika yanakutana kule Zanzibar na idadi iliyokuwa inatarajiwa ni kama Waheshimiwa Wabunge 300 kutoka nchi mbalimbali za Afrika za Gambia, Nigeria, Ghana, Sierra Leone, Zambia, South Africa, Namibia, Zimbabwe, sisi wenyewe, Rwanda, Uganda, Kenya na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka jana nilipokuwa naondoka kule *enrollment* ilikuwa zaidi kidogo ya mahudhurio ya Waheshimiwa Wabunge 600 yaani *double*. Ni mkutano ambao hujawahi kuhudhuriwa kwa kiwango hicho kwa miaka mingi sana. Kwa kweli nchi yetu inapendwa na watu wana imani na nchi yetu. Ndiyo maana kumekuwa na mahudhurio makubwa ya kihistoria katika mkutano ule. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, agenda ya mkutano huu ni hiyo hiyo *e-Parliament*, jinsi ambavyo Mabunge ya Afrika sasa yamekwenda mbali katika *e-Parliament*. Wanasi mama Maspika wenzangu wanazungumzia mambo yao yalivyo mimi hata kunyanya kichwa siwezi kwa sababu sisi hata hatua moja hatujaanza.

Waheshimiwa Wabunge, alikuja Spika wa Rwanda hapa wakati ule tu karibu tunamaliza karbu tunamaliza kipindi cha bajeti, nilipompitisha humu ndani alishangaa kuona marundo ya makaratasi, akauliza ninyi vipi hapa? Nikamwambia ndiyo Bunge letu. Akaniambia Bunge la

Rwanda hamna karatasi hata moja, Kenya ni hivyo hivyo, Uganda wako mbali, sasa hatuwezi sisi kuwa wa mwisho katika kila jambo, sasa tunasema angalau tuanze na *Order Paper* tu peke yake, hiyo moja tu sio *documents* nyingine. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa hata hiyo hatua moja na yenyewe nayo tuwe tunasuasua? Tutaanza na tunaanza kesho, wewe lete *emails* zako hapa mezani, kila kitu wewe lete hapa, usipoweza kuleta hapa peleka kwa Katibu tutakutumia na utaipata mapema kabisa asubuhi popote pale ulipo. Kama kuna Mbunge hamudu *bundle*, sasa hilo jambo tena, mbona *bundle* za mambo mengine tunaweza jamani, tutamudu tu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mambo ya *WiFi* na kadhalika tutarekebisha *as we go on* lakini tuanze mahali. Hili jambo lina faida nyingi, kwa mfano, sasa hivi ukiwa haupo hapa Bungeni unakuwa hujui *almost* kila kinachoendelea lakini hata ukiwa Jimboni kupitia simu yako utakuwa unajua kitu gani kinaendelea, nini kikoje, *paper* gani imeingia, unapata *information* popote pale ulipo. Itawezesha hata tutakapokuwa hatupo, Wizara labda ina jambo fulani kuhusu Kamati fulani wanawaaletea *information* kupitia mitandao yenu moja kwa moja, itarahisisha sana mawasiliano.

Waheshimiwa Wabunge, *documents* nyingi tunaziacha hapa Dodoma lakini kupitia mtandao tutaondoka na *documents* zetu zikiwa kwenye mtandao, kwa hiyo, popote pale ulipo unaangalia. Faida zake ni nyingi kuliko huu utaratibu wa makabrasha ambayo mengi yanaachwa humu ndani, mengine kwenye *pigeonhole*, wengine wanayaacha kwenye gesti huko na kadhalika. Kwa hiyo, kidogo kidogo, hatusemi tutaenda haraka, hapana, tutakwenda kidogo kidogo lakini mwisho wa siku tutakuwa tumeenda mbali zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, ni kweli sio kwamba tumefuta mpango wa kuwa na *iPad*bado tunaendelea nao lakini tutake tusitake kwa kweli simu ya kiganjani ndiyo kitu

ambacho mtu yuko nacho muda wote na mahali popote. Siku hizi hata ukiwa na *desktop* ni kama haina kazi kwa sababu ukishakuwa na simu ya mkononi ni kila kitu. Kwa hiyo, twende na dunia na *advancement* ya mambo yanavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambaao labda kidogo kuna shida ya ufuatiliaji, wale Wasukuma na Wanyamwezi, wanione tu. Akina Mheshimiwa Musukuma wenye simu vimeo wanione tuone tunafanyaaje lakini kwa kweli kila Mbunge lazima awe na *android phone* kwa maana ya kupata mawasiliano ya Kibunge na wapigakura. Haiwezekani wapigakura wanataka kukuletea *information* wewe simu yako haipokei. Katika dunia ya leo hiyo haikubaliki.

Naomba tulipokee hili la hiki kimoja tujaribu. Usipokuwa katika mawasiliano hayo kipindi cha maswali na majibu hutaweza kufuatilia chochote. Kwa hiyo, naomba sana sote kabisa simu zetu tuwe nazo kuanzia kesho asubuhi. Katibu, umesikia? Karatasi ya *pink* ni marufuku kuanzia kesho, hakuna karatasi ya *pink* kuingia hapa ndani. (*Makofi*)

Katibu tuendelee.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI

AZIMIO LA BUNGE

Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo

SPIKA: Ahsante sana. Moja kwa moja sasa nimuite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, karibu tafadhalii. (*Makofi*)

MHE. MUSSA A. ZUNGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kulileta Azimio hili hapa Bungeni, Azimio muhimu kwa Taifa letu na kwa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika, *Southern Africa Development community (SADC)*.

Mheshimiwa Spika, Waasisi wa Taifa letu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume, walitamani kuona kuwa Bara lote la Afrika linakuwa huru kutoka kwa Wakoloni. Ni kutokana na matamanio hayo, tangu nchi yetu ijipatie uhuru wake mwaka 1961 na baadaye kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume walikuwa mstari wa mbele kuendeleza harakati za ukombozi ili kuhakikisha kuwa nchi zote za Kusini mwa Afrika zinakuwa huru. Aidha, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisisitiza kwa kusema kuwa uhuru wa Tanzania hauna maana kama nchi nyingine za Afrika haziko huru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na dhamira hiyo iliyochagizwa na uzalendo wa *Pan Africanism*, muasisi wa Taifa letu alikubali Makao Makuu ya nchi zilizo mstari wa mbele katika ukombozi Kusini wa Afrika yawe nchini Tanzania Jijini Dar es Salaam. Aidha, alikubali Katibu Mkuu wa harakati za ukombozi atoke Tanzania ambaye alikuwa ni Marehemu Brig. Hashimu Mbita. Dhamira hiyo ilipelekeea Tanzania kuwa na kambi za wapigania uhuru kutoka nchi mbalimbali za Kusini mwa Afrika zilizokuwa chini ya makucha ya ukoloni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika - *Southern Africa Development Community (SADC)* mwaka 1980 ni kutokana

na mchango mkubwa uliotolewa na nchi yetu ya Tanzania. Baada ya kuanzishwa kwake, viongozi wa nchi hizi wamekuwa wakifanya mikutano yao mwaka hadi mwaka. Mwaka huu 2019 mikutano ulifanyika Jijini Dar es Salaam Tanzania. Kauli mbiu ya mikutano huu ilikuwa ni mazingira wezeshi ya biashara na viwanda kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, mikutano huu umekuwa na manufaa na mafanikio makubwa sana. Hii ni kwa sababu Mheshimiwa Rais alipanga masuala mbalimbali yenye manufaa kwa nchi za *SADC* na nchi yetu kama ifuatavyo:-

(i) Aliagiza maonesho ya wasanii, hususani wauzaji wa vinyago wakaoneshe na kuuza bidhaa zao pembezoni mwa barabara zote zilizo karibu na ukumbi wa mikutano. (*Makofii*)

(ii) Alimpangia Mheshimiwa Rais wa Afrika Kusini, Mheshimiwa Cyril Ramaphosa kutembelea iliyokuwa kambi ya wapigania uhuru wa Afrika Kusini ya Mazimbu Mkoani Morogoro. Baada ya kutembelea Kambi hiyo, Mheshimiwa Cyril Ramaphosa aliahidi kujenga Kituo cha Utalii katika eneo hilo na kuifanya lugha ya Kiswahili kutumika katika nchi yake. (*Makofii*)

(iii) Alishauri kuwa kuwa na maonesho ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda kutoka nchi za *SADC*. Maonesho haya yameweza sekta binafsi nchini kupata fursa mbalimbali nje ya nchi.

(iv) Alinadi vivutio vya utalii vilivyopo nchini na hivyo kupanua wigo wa utalii nchini.

(v) Alihimiza nchi za *SADC* kutumia vizuri rasilimali zake kwani ndiyo urithi wa pekee kwa wananchi wa nchi za *SADC* na kukemea ufisadi katika Afrika hususani Ukanda huu wa *SADC*.

(vi) Alihimiza kupunguza vikwazo vya biashara na urasimu usio wa lazima katika uwekezaji na ufanyaji wa biashara kwenye eneo la nchi za *SADC*.

(vii) Alisisitiza nchi za *SADC* kuimarisha viwanda vyake ili kuweza kuzalisha bidhaa ambazo wanachama watashirikiana katika kununua na kuuza ndani ya nchi za *SADC* badala ya kuagiza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uongozi wake wa kizalendo, wananchi wengi katika mataifa mengi ya Afrika wanapenda kuwa na viongozi wa aina ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mwanzoni mwanazuoni mmoja kutoka nchini Kenya, Profesa Patric Lumumba katika moja ya mihadhara yake ya Kimataifa alitamani kitu kinacholtwa *Magallification of Africa* akimaanisha kuwa Bara la Afrika lioneze kwa namna Magufuli anavyoiongoza Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa nchi za *SADC*. Azimio hili linatolewa chini ya Kanuni ya 54 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA tangu aingie madarakani, Mataifa mengi yamekuwa yakipendezwa na uongozi wake;

KWA KUWA viongozi wa Nchi za *SADC* wanatambua na kuthamini uongozi bora wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli;

KWA KUWA kutokana na kutathiminiwa na kuaminiwa na viongozi wote wa Nchi za *SADC*, kwa umoja wao waliamua kumpa Uenyekiti Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli;

KWA HIYO BASI Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Sita, Kikao cha Kwanza tarehe 6 Septemba, 2019 linaazimia kwa kauli moja kama ifuatavyo:-

- (i) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika *SADC*. (*Makofi/Vigelegele*)
- (ii) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuwashawishi Marais wote wa nchi 16 za nchi za *SADC* kukubali Kiswahili kiwe lugha rasmi itakayotumika katika shughuli mbalimbali za Jumuiya hiyo. (*Makofi/Vigelegele*)
- (iii) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kusimamia maandalizi mazuri yaliyofanikisha ufanisi mkubwa katika uendeshaji wa mkutano huo. Maandalizi hayo yalihusisha usafiri wa ndani, malazi na usalama kwa wageni wote hususani Marais wa nchi za *SADC*. (*Makofi*)
- (iv) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kusimamia uratibu na kuendesha vyema vikao vyote katika mkutano wa Marais wa Nchi za *SADC*. (*Makofi/Vigelegele*)
- (v) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuwezesha na kuratibu utiaji saini wa itifaki zenye maslahi kwa nchi za *SADC*. (*Makofi*)
- (vi) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kutoa wito kwa nchi wanachama kuimarisha viwanda vyao ili kuweza kuzalisha bidhaa ambazo watashirikiana kwa kununua na kuuza ndani ya nchi za *SADC* badala ya kuagizia kutoka nje. (*Makofi*)

(vii) Kuitaka Serikali kuweka mazingira wezeshi ili Watanzania wengi waweze kutumia fursa zinazoweza kupatikana kutoka nchi za *SADC*.

(viii) Kuitaka Serikali kuanzisha Kitengo Maalum kitakachokuwa kinatoa taarifa za mara kwa mara kuhusu fursa zinazopatikana katika nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawaita wachangiaji na tutachangia kwa dakika zisizozidi tano. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa *SADC*. Nina sababu tatu za kuunga mkono Azimio lilioko mbele yetu. Kwanza Azimio hili linatukumbusha historia ya ukombozi Kusini mwa Bara la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mtakumbuka mwaka 1960 mpaka 1980 Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alijaongoza viongozi wenzake kuunda Umoja wa Nchi zilizo mstari wa mbele kwa ukombozi Kusini mwa Afrika na hatimaye kuundwa kwa Jumuiya ya *SADC*. Viongozi hao ni Agostinho Neto wa Angola, Marehemu Khama wa Botswana, Kenneth Kaunda wa Zambia, Samora Machel wa Msumbiji na Mzee Robert Mugabe wa Zimbabwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa aliiatumia ardhi ya Tanzania rasilimali alizotujalia Mwenyezi Mungu katika kuendeleza mapambano ya kudai uhuru Kusini mwa Afrika. Pamoja na umasikini wa Tanzania Baba wa Taifa alijitahidi na kutoa mchango mkumbwa sana, lakini kwa bahati mbaya wako baadhi ya watu wanadhani kwamba mchango alioutoa Baba wa Taifa katika kupigania uhuru haulingani na hadhi anayopewa Baba wa Taifa katika baadhi ya nchi Wanachama. Ni matarajio yangu kwamba kufanyika kwa mkutano huu katika ardhi aliyozaliwa Baba wa Taifa kutatukumbusha historia iliyo tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pili azimio hili linatukumbusha kwamba ajenda ya ukombozi Kusini mwa Afrika na Afrika kwa ujumla bado haijakamilika. Waafrika tusipokuwa makini, siku moja tusishangae, ukoloni mamboleo unaweza kurudi katika Bara la Afrika. Ni wajibu wetu tufanye kila linalowezekana tushirikiane kulinda uhuru huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatu, Azimio hili linasisitiza juu ya umuhimu wa nchi za *SADC* kuendeleza awamu ya pili ya agenda ya mapinduzi na Uhuru wa Kiuchumi katika Jumuiya hii ya Afrika ya Mashariki. Kwa kuwa harakati za kupigania uhuru katika awamu ya kwanza ziliratibiwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni matarajio kwamba awamu ya pili ya mapambano ya Uhuru wa Kiuchumi yataratibiwa tena hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge na kama wawakilishi wa Watanzania, ni matarajio yetu kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hataongoza mapambano haya ya ukombozi wa kiuchumi. Nalisema hili kwa sababu ipo dhana na hata Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wakati wa Mkutano alisema wazi kwamba yapo baadhi ya Mataifa wanachama wa *SADC* yanafanya biashara kubwa zaidi na nchi zilizoko nje ya Jumuiya kuliko zinazofanya ndani ya Jumuiya. Nafikiri jambo hili halikubaliki hata kidogo. (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio la Bunge. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Nilishakutaja Mheshimiwa Amina Makilagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami kwa niaba ya wanawake wenzangu walioko ndani ya ukumbi huu na wanawake wa Tanzania ambao sisi Wabunge wanawake wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunawawakilisha, napenda kuunga mkono azimio hili lilitowasilishwa asubuhi ya leo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kwanza naunga mkono azimio hili la kumpongeza Rais kwa sababu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikubali kwa niaba ya Watanzania kwamba Mkutano huo wa *SADC* ufanyike nchini Tanzania ambako ni heshima ya Watanzania wote na ikiwa ni ishara tosha ya kumuenzi baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hayati Mzee Karume.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio hili kwa sababu ni ukweli usiopingika Mkutano wa *SADC* uliandaliwa vizuri chini ya uongozi wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli mkutano huu ulitupa hadhi na heshima Watanzania kuendelea kuwa *champion* wa ukombozi wa Bara la Afrika ikiwemo nchi za *SADC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono, azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu amepokea kijiti hiki cha

kuwa Mwenyekiti wa *SADC* kutoka kwa Rais wa Namibia ikiwa nchi ya Tanzania na nchi za *SADC* tukiwa na amani na usalama. Ninapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio hili la kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na si mwingine ni kipenzi chetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliongoza vema Mkutano wa *SADC* haijapata kutokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa sababu kupitia Mkutano wa *SADC* Rais wetu kipenzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishawishi Marais wenzake na wakakubali lugha ya Kiswahili, lugha ambayo ni tunu ya Tanzania iwe sasa ni lugha ya nne katika nchi za *SADC*. Haijapata kutokea na katika hili hatutakaa tumsahau Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuleta azimio hili tumpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kweli tunampongeza na tunakushukuru sana. Naunga mkono azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ameendelea kushawishi Marais wenzake na nchi za *SADC* ziendelee kujitegemea kiuchumi kwa kutumia rasilimali zake ili nchi za *SADC* ziondokane na utegemezi; na akanukuu akasema, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na pale alipopumzika alisema kujitawala ni kujitegemea na mtaji wa masikini ni nguvu zake mwenyewe; na uwezi kuwa uhuru kama nchi yako haijitegemei. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kusisitiza nchi za *SADC* kujitegemea na yeye mwenyewe akawa ndiyo mfano wa kuifanya Tanzania sasa ijitegemee na mfano hata wa bajeti hii, tulikuwa ni tegemezi kwa asilimia 40. Sasa Tanzania tunajitegemea kwa asilimia nane. Hiyo peke yake tuna kila sababu ya kutaka kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naunga mkono azimio hili, hongera sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Wanawake wa

Tanzania tunakupongeza tuko pamoja na wewe. Ninachokuhakikishia, uchaguzi wa 2020 kura zote ni zako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio hili. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami kama wenzangu waliotangulia, naunga mkono azimio hili lilitololekwa mezani. Azimio hili linatukumbusha historia ya ukombozi katika Afrika. Tanzania iliongoza nchi za Kusini mwa Afrika ili nchi ambazo hazijapata uhuru zipate uhuru Mwalimu Nyerere akiwaongoza. Tulianza na Mlungushi *Club* ambayo alikuwa analiwa akiwaongoza Mwalimu Nyerere, lakini Mabeberu wakaipiga vita nchi nyingine zikawa zinajipendekeza kwa mabeberu, ndiyo Mwalimu akaanzisha nchi za mstari wa mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya nchi za mstari wa mbele zipo nchi zilikuwa zinajitegemea Afrika Kusini kiuchumi. Kwa hiyo, Mwalimu akaona afadhali aache mstari wa mbele, ndiyo ikaazishwa *Southern African Development Coordination Conference* ili hizi nchi za Kusini mwa Afrika zisianze kujitegemea kijuchumi, ziachane na Afrika Kusini. Baada ya kuanzisha hii *Southern African Development Coordination Conference*, nchi za Ulaya na Marekani zikaanza kutambua kundi hili, likaanza kumpa *pressure* Afrika Kusini iachane na ubaguzi. Ndiyo ikakua ikaanza *Southern African Development Community* yote hii iklongozwa na Mwalimu Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vijana wa sasa wakitaka kuelewa Mwalimu Nyerere alikuwa *champion* wa uhuru katika Afrika, wasome kitabu chake cha *Crusade for Liberation*, utaona Mwalimu alivyojitoa ili Afrika yote ipate uhuru. Kuwepo kwa *Southern African Development Community* ndiyo kumeleta ukombozi Zimbabwe na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais. Marais hawa waliokuja kwenye mukutano wa juzi, Rais Cyril Ramaphosa na Rais Mnangagwa angalau wanatambua umuhimu wa Tanzania kuleta mkombozi Kusini mwa Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado kwenye mukutano huo Tanzania ikiongozwa na Rais wetu pamoja na Waziri wa Mambo ya nchi za Nje inaendeleza mapambano ya kuikomboa Zimbabwe ili vikwazo viondolewe na Zimbambwe. Bado Tanzania iko... (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Azimio hili ni nzuri sana linatukumbusha *Champion* wa Tanzania katika kuikomboa Afrika. Yote haya ni mazuri, naunga sana mkono, nasema, *boseaga maswano muno muno munze yetu. Muaha yalumbwe. Sendenyi.* (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana Victor. Mwaha yalumbwe, sandenyi.

Nilimtaja Mheshimiwa Ally Saleh na atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kwanza kusema kwamba siyo tatizo kuona fahari kuona fahari kwamba Rais wako anakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya kubwa katika Kanda au popote pale. Hiyo siyo *issue*, kwa sababu ni *rotationally*. Vyovyyote vile angekuwa mwingine ye yote angeweza kuwa Mwenyekiti kesho, kesho kutwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema *you should not politicize the issue, twende sober mind, tutazame nini tumshauri* Mheshimiwa Rais wetu katika hicho kipindi anachokuwa Mwenyekiti, tutafanya nini kama Tanzania? Cha muhimu, tufanye ili *legacy* yake iwe na maana zaidi na siyo kumpongeza wakati baadaye hatafanya kitu cha maana, ili *legacy* yake ikumbukwe zaidi ya kuwa Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sisi ni *member* wa *SADC*, lakini katika mukutano ambao ni wa mwisho kabla Mheshimiwa Rais kuwa Mwenyekiti Serikali yetu imeshindwa kipeleka Wabunge kwenye Mkutano wa *SADC* uliokuwa Mozambique. Vile vile sisi tukiwa Wabunge wa *SADC* tumeshindwa katika mikutano mitatu kuhuduria katika mikutano ya *SADC*. Picha hii haiwezi kuwa nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi tuna mukutano hapa kwetu, lakini kuna utamaduni wa *SADC* wa kukaribisha *NGOs*, tunaambiwa kwamba wana-*NGOs* wengi walikuwa *harassed* walipokuwa Dar es Salaam; wakasachiwa wakapekuliwa wakafanyiwa kila kitu. Sisi kama *SADC* tuna itifaki ya kufanya *election observations*, lakini katika mikutano uchaguzi kibao hatuendi, tunacha *legacy* gani kama Taifa? Kuna *Model Laws* na *visions* za *SADC* ambazo zinataka nchi zifanane kwa kadri inavyowezekana. Kama nchi hatufanyi vizuri katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *SADC* inajengwa kuwa Bunge kamili baadaye. Tungeomba Rais wetu asaidie watakuja baadaye katika Bunge lingine walikute Bunge la *SADC* limekaa sawa sawa, *role* yake iwe nzuri hiyo.

Mheshimiwa Spika, cha pili, nakuja kwenye uwekezaji. *SADC* ina watu karibu 370 wengine wanasema 350 jumla yake, wana *GDP* ya milioni 6.07 kwa pamoja, lakini pia *SADC* inasemekana kwamba ina-perform low by 25 percent ya uwezo wake, kwa maana bado biashara mionganini mwetu iko ndogo sana. Kwa mfano, Tanzania tunafanya vizuri na *South Africa* pengine na *Democratic Republic of Congo*, lakini sisi kama Taifa hatufanyi vizuri na nchi nyingine. ... Katika hili tulifanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia kama *zone* hii kuna tatizo kubwa la *zone phobia South Africa*. Hii inafanya kusiwe na uzuri wa nchi nyingine kushiriki baina yao pamoja. Tungemshauri Rais wetu hili alisimamie vizuri ili *zone phobia* na kufungua mipaka kuwe kuzuri na kwa Mataifa yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kusema kwamba tumefurahi kwamba Rais wetu amekuwa Mwenyekiti wa *SADC*, ni mwaka mmoja tu, lakini muhimu *legacy* gani ataacha ili tuje tufurahi kama Watanzania ametufanya chema kwa ajili ya nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Peter Serukamba, utafuatiwa na Mheshimiwa Agness Marwa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuunga mkono azimio lilioletwa leo asubuhi. Kwanza nami nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwanza kwa kukubali mukutano kufanyika Tanzania. Ni kweli mukutano ya *SADC* ni *rotational* lakini angeweza kukataa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kama hali yetu ya pili isingekuwa nzuri, bado hata wenyewe watu wa *SADC* wasingeleta mukutano Tanzania. Kwa hiyo, ni vizuri tuelewe mukutano umekuja Tanzania kwa sababu ya utayari wa Rais wetu, ulikuja kwa sababu Tanzania tupo tayari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa sababu kwanza kama walivyosema wenzangu, Tanzania ndiyo kitovu cha ukombozi wa Bara la Afrika hasa upande wa Kusini mwa Afrika; na kwa wale mnaokumbuka, wakati wa *liberation struggle*, ile *committee* ya *liberation struggle*, Katibu Mtendaji wa kwanza alikuwa Marehemu Balozi George Magomba baadaye akafuatiwa na Ndugu *Brigadier* Hashim Mbita. Kwa hiyo, Tanzania tumefanya kazi kubwa sana kwa ukombozi wa Kusini mwa Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na nikiomba Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wetu mpya wa *SADC*, kazi ya ukombozi Kusini mwa Afrika imekwisha, nadhani umefika wakati na Rais amesema huu ni wakati wa ukombozi wa uchumi wa Kusini wa Bara la Afrika. Nina uhakika Mheshimiwa

Rais Dkt. Magufuli atalisimamia hili kama Mwenyekiti mpya wa *SADC* kuhakikisha tunaondoa vikwazo vyta kufanya biashara kati ya nchi wanachama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alipokuwa anafungua Bunge la *South Africa* mwaka 1994 aliwaambia wa *South Africa* msijigeuze kuwa kaka wakubwa, *South Africa* hamna jirani, jirani yenu ni sisi Waafrika wenzeni. Akasema ili *block* hii iweze kuendelea, lazima tufanye biashara ndani ya wanachama wenye. Kwa hiyo, ni matarajio yangu na ninayo hakika Mwenyekiti mpya wa *SADC* atafanya yafuatayo: moja, akisaidiwa na Waziri wa Mambo ya Nje kuhakikisha tunaondoa vikwazo vyta kufanya biashara ndani ya nchi wanachama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pili, ili tuweze kufanya biashara na wananchi wanachama, umefika wakati lazima tutafakari, hivi kwenda Kongo ni lazima niwe na *visa*? Hivi Mkongoman lazima awe na *visa* kuja Tanzania? Hivi Wamalawi lazima wawe na *visa* kuja Tanzania? Tukifanya hivyo, nina hakika biashara kwenye nchi hizi itashamiri na ninayo hakika hii ndiyo itakuwa *legacy* atakayoiacha Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza kwa sababu mukutano wenye umefanyika kwanza kwa utulivu mkubwa sana, lakini pia umefanyika kwa ushirikishwaji wa watu wengi sana. Kwa mara ya kwanza mukutano wa Kitanzania; na ninawapongeza walioandaa mukutano huu, tumeona *private sector* ikishiriki kuhakikisha mukutano huu unafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nami nashukuru sana na ninamtakia mema Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa hiyo aliyoianza. Moja *legacy* ya kwanza kama mnavyofahamu Bunge hili, kazi ya kwanza Rais amefanya kwenye *SADC* ni kufanya Kiswahili ni kuwa lugha ya *SADC*. Kwa hiyo, mtu ye yeyote mwenye wasiwasi wa *legacy* ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwenye *SADC*, *legacy* ya kwanza ni Kiswahili. Ninaamini *legacy* ya pili itakuwa ni biashara ndani ya nchi ya wanachama na *legacy* ya tatu

nina hakika itakuwa kuhakikisha katika nchi za *SADC* kunakuwepo na utulivu na amani kama ilivyo Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba niunge mkono azimio hili. Namtakia maisha mema Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti mpya wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agness Marwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *SADC*. Hii ni heshima kubwa kwetu kama Wabunge, lakini ni heshima kubwa kwa Watanzania na nchi kwa ujumla. Mimi niseme hii nafasi sasa imempata mkunaji maana sasa imefika mahali pake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu ameanza vizuri. Ukweli ni kwamba Watanzania bado lugha ya kigeni Kiingereza na lugha nyingine, zilikuwa ni lugha ambazo zilikuwa zinaleta shida sana kwenye mikutano na sehemu mbalimbali kutokana na kwamba ni lugha ambazo tulikuwa hatuzijui vizuri, tulikuwa hatufundishwi tangu utotonii. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, niungane na Mbunge mwenzangu kusema kwamba ni kweli atakuwa ameacha *legacy* katika Jumuiya hii ya *SADC*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kwa Tanzania tumekuwa mstari wa mbele chini ya uongozi wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika harakati za kutafuta uhuru wa baadhi ya nchi za *SADC*. Kwa kweli

tumewasaidia nchi nyingi sana kiasi kwamba Uenyekiti ulipofikia umefikia mahali pake, kwamba nasi sasa tuonekane kwa yale tuliyoyafanya, kwamba sasa hivi tunaweza kufanya kitu gani.

Mheshimiwa Spika, sina shaka sana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi alioupara wa *SADC*, kwa sababu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli naamini kabisa ataondoa ukiritimba katika masoko ya biashara. Kwa mfano, kule kwangu Mkoani Mara unaweza ukafanya biashara ama za nafaka au biashara ya dagaa niliyokuwa naifanya mimi kutoka nchini kwetu kuvuka mpakani kunakuwa na ukiritimba lakini kunakuwa pia na masuala ya rushwa. Sasa naamini kabisa chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli rushwa itakoma na hizo nchi washirika naamini kabisa watamtambua kwamba huyu ndiyo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais wetu ni kati ya vivutio na hasa katika nyanja ya uongozi, kwa sababu ni kiongozi bora, ana uongozi uliotukuka, Wabunge pia tumeiga kutoka kwake, mfano; Kama unakumbuka safari hii likizo ya Bunge liliopita kila Mbunge amekuwa akifanya kazi na hii yote ni kutokana na uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwamba asiye fanya kazi na asile na ambaye hajafanya kazi kwa kweli kuliona hili Bunge mwaka 2020 asahau. Kwa hiyo, huu uongozi safari hii umempata mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa hili suala la viwanda maana yeye alipochaguliwa tu alisema kaulimbiu yake ni Tanzania ya Viwanda, lakini kumbe ni Rais ambaye ana maono makubwa na ndiyo maana tunasema tumepewa Rais ambaye ametoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu hapohapo ukiangalia imeunganishwa kwamba sasa *SADC* pia wameongelea suala la viwanda na kukubaliana. Hivyo, naamini kabisa viwanda sasa vitakuwa vingi sana, **mfano wake nimwambie hata Mheshimiwa Neema Mgaya Kile kiwanda chake cha vyerehani Kumi** sasa akianzishe kwa

sababu haya mambo yote yanafanyika kutokana na makubaliano ya *SADC*.

(Maneno hayo yalifanyiwa marekebisho na Mheshimiwa Neema W. Mgaya na kusomeka Vyerehani 370 vyenye na siyo Vyerehani Kumi)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wabunge wenzangu au wapiga kura wangu wa *NEC* ambaao ndiyo Wabunge, pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Mara, na hasa Wabunge wa CCM, napongeza sana kwa kweli uongozi huu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, imani yangu ni kwamba sasa atafanya mabadiliko makubwa na watauona uongozi wake uliotukuka ambaao Tanzania tunajivunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Agness Marwa.

Waheshimiwa Wabunge kesho mchana Mheshimiwa Agness atakuwa anambatiza mtoto wake mchanga kwenye *Chapel* ya Bunge hapa, kwa hiyo mnakaribishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, sasa uhitimishe hoja yako tafadhali, una dakika zisizozidi Kumi. (*Makofi*)

MHE. MUSSA A. ZUNGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru tena na kuwashukuru Wabunge Sita waliochangia ambaao ni Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Peter Serukamba, tumemalizia na Mheshimiwa Agness Marwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ameunga mkono na ametoa *history* ya namna *Frontline States* ilivyoanzishwa, ni kweli ziliikuwa ni nchi Tano ni kama vile alivyozisema Tanzania, Botswana, Angola, Msumbuji na

Zambia. Ameunga mkono na ameendelea kusema kuwa nchi hizi sasa zikumbuke namna Tanzania ilivyojitoa na tuendeleze kujitoa kuhakikisha sasa tunajitoa kwenye masuala ya uchumi. Mheshimiwa Makilagi nae ameunga mkono, amezungumzia namna Mheshimiwa Rais alivyozungumza kwenye hotuba yake tujitegemee. Mheshimiwa Victor Mwambaliaswa ameendelea kutoa *history* kabisa ya namna Mwalimu alivyopambana na kuzungumza utawala wa kibeberu Afrika uondoke.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ally Saleh naye amepongeza, amezungumza kuhusu namna ushiriki wa Tanzania kwenye Mabunge haya. Hata hivyo, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Ally Saleh Wabunge wetu wanashiriki kwenye mikutano ya Bunge la Afrika na hata Makamu wa Rais wa Bunge hilo la Afrika anatoka Tanzania, kwa hiyo hii inaonesha Wabunge wetu wanakwenda na wanashiriki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peter Serukamba ameunga mkono, amezungumzia masuala ya uchumi, amepongeza na suala la utilivu wa nchini mwetu, amesisitiza kwa suala la sekta binafsi nayo itiwe mkazo na amezungumzia, amekumbusha kuwa *legacyya* Mheshimiwa Rais katika SADC katika mambo yote lakini haitasahahulika kwa Kiswahili kimeweza kuwa kitatumika na kitaweza kukua.

Mheshimiwa Spika, watu lazima wakumbuke Tanzania tunapotoka. Kama mtakumbuka tarehe 11 Novemba, 1965 Rhodesia chini ya Ian Smith walitangaza *UDI* (*Unilateral Declaration of Independence*), Tanzania ilikuwa ni nchi ya kwanza kupinga utawala huu dhalimu na Tanzania wakaomba Uingereza wasiitambue Serikali ya Ian Smith ya Rhodesia, lakini Harold Wilson wakati ule akiwa ni Waziri Mkuu wa Uingereza walikataa na palepale Mwalimu Nyerere akavunja uhusiano na Uingereza. Kuonesha namna gani gani Rais Nyerere alikuwa na uchungu na ukombozi wa Afrika, tulikataa misaada kutoka Uingereza. Hii inaonesha namna Tanzania ilivyokuwa mstari wa mbele katika kupambana na udhalimu wa nchi hizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilichelewesha maendeleo yake ili kuhakikisha nchi za Afrika zipate uhuru wake, kwa hiyo damu ilimwagika na watu wengi walipoteza maisha yao. Sasa tunaliagiza kwenye Azimio letu na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kufuatilia hasa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha *trading within block* ya SADC inafanywa na tuna-trade kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha sasa hivi ndani ya Afrika tuna-trade kwa asilimia 16 tu, tofauti na nchi za Ulaya zina-trade kwa asilimia 70 wenyewe kwa wenyewe. Ili tujikomboe lazima tuanze kutafuta masoko ya ndani ya kujikombua na kuhakikisha bidhaa zetu za kilimo na bidhaa zetu nydingine zinanunuliwa na Waafrika wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru, na sasa niwaombe Wabunge wote kwa pamoja kwa Kambi zote ambazo ziko ndani tuunge mkono azimio hili na tumpongeze Rais wetu kuchukua nafasi ya kijiti hiki na inawezekana akaendelea tena kuchukua kijiti hiki kwa mwaka mwingine unaokuja kutokana na kazi nzuri anayoifanya na kutokana na nchi za Afrika kumkubali na kumtegemea ye ye kutoonga wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, nawaashukuru sana kwa kuunga mkono hoja. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba niwahoji kuhusiana na Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya SADC.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na kuendesha vyema Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo lilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wote wameafiki. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa Azimio hili muhimu ambalo linaweka historia ya Bunge letu katika kuunga mkono jambo hili muhimu sana katika maendeleo ya Jumuiya yetu ya SADC. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na kupitia yeye piatunapeleka salamu kwa Maafisa wote wa Serikali waliohusika na jambo hili wakiwemo Mawaziri wote mliokuwa mnapokea wageni na kuwasindikiza na mliokuwa na *roles* mbalimbali katika kufanikisha mkutano huu. Tunasema mmetutoa kimasomaso, mmetubeba. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna wengine inabidi tuwataje kidogo kwa kweli walijitokeza zaidi, Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje kama Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa SADC tunakupongeza sana na wewe kwa *role* yako mpya hiyo tunakutakia kila la kheri, ulifanya kazi kubwa sana, pia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kwa kweli pamoja na ugeni wake alijitahidi kweli, aliandaliwa makongamano mengi, walitembelea viwanda vyetu na kadhalika. Pia Mawaziri wengine wote siwezi kuwataja wote kwa wakati mmoja, wote tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia, nami kama Mbunge wa Kongwa niwakumbushe kidogo tu Wizara ya Mambo ya Nje. Kila wakija wakubwa hawa hasa kutoka *South Africa* wao huwapeleka Mazimbu, sasa hapa hatukatai lakini tunasahau historia. Nafikiri wale mlioona mitandaoni mliona yule Mama mmoja pale Morogoro, yule Bibi aliyeenda kwenye kaburi la Mume wake anayetwa Oscar aliyekuwa mpigania uhuru wa *South Africa*. Baada ya haya mambo ya Rhodesia aliyelezea Mheshimiwa Mussa A. Zungu 1965, Mkutano wa

AU uliofuatia wakati huo ikiitwa *OAU*, walikubaliana kwamba sasa habari ya maneno maneno katika ukombozi haisaidii, lazima tuendane na lugha ambayo Mkoloni au Kaburu anaielewa na lugha peke yake waliyokuwa wanaielewa ni lugha ya silaha. Kwa hiyo, wakakubaliana kuanzisha mapambano rasmi.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo ilipokubalika pale Marais watatu wakaja kuanzisha kambi ya kwanza kabisa ya mapambano ya ukombozi, Rais wa Algeria wakati huo, Rais wa Misri wakati huo Gamal Abdel Nasser na Mwalimu Nyerere, mwaka 1967 Marais hawa watatu walikuja Kongwa. Wakatua pale Kongwa kwenye uwanja wetu mdogo na ndege zao zote, ilikuwa kivumbi wengine tulikuwa wadogo sana lakini tunakumbuka tulichokiona, ndiyo walioanzisha Kambi ya Kongwa, Kambi ya Kongwa ndiyo walikaa Vyama vyote vya nchi zote Tano, walikaa wa *South Africa*, Msambiji, Zimbabwe, Namibia na Angola. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, Mazimbu hawakukaa nchi Tano, hakuna kambi nyininge yoyote waliokaa nchi zote Tano, Mazimbu hapakuwa ni mahali pa *combat*, Mazimbu pale ilikuwa ni mambo ya *training* wakati huo karibu uhuru unapatikana ili watu wafundishwe wakipata uhuru watakuwa *Administrators* na nani ndiyo wakasogezwa karibu na mjini pale, lakini Kongwa ilikuwa mahali pa shughuli ya ukombozi (*combat*). Kwa hiyo, tunasahau historia tunaanza kufanya vitu vingine kidogo siyo sawasawa sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, pia yule Mama aliyejitozeza, hawa watu walipata wenzao na wengi wao Kongwa, baada ya uhuru watoto wengi walichukuliwa wakaenda Namibia, wapi na wapi, lakini akina mama wa Kitanzania wao walibaki, walipohamia Mazimbu walichukua familia zao toka Kongwa wakaja Mazimbu lakini baada ya uhuru wale wanaume wakaenda na watoto wakaenda, akina mama wakabaki. Sasa hawa wanapokuja kusalimia na kuangalia makaburi ya ndugu zao hata kuwasalimia wale akina Mama hakuna, sasa hii kwa kweli! Wakati nao walitoa huduma muhimu. (*Kicheko/Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo hii historia ya sasa kwa sababu sisi ni Wenyekiti wa SADC inabidi tuiweke vizuri ikae sawasawa. Tulichangia mambo mengi sana, siyo tu damu na nini, lakini kuweka wapigania uhuru katika mazingira ambayo kwa kweli na wanakumbuka mpaka leo, ndio maana Rais wa kwanza wa Msumbuji Samora Machel alikaa Kongwa, aliyefuata, Joaquim Chissano alikaa Kongwa, aliyefuata alikaa Kongwa, huyu wa sasa hivi ye ye alikaa Nachingwea. Halafu Rais wa Namibia wa Kwanza alikaa Kongwa, aliyefuata, Hifikepunye Pohamba alikaa Kongwa, huyu wa sasa hivi alikaa Kongwa, tukiendelea historia ya Kongwa ni kubwa lakini inawekwa pemberi katika suala hili la ukombozi na sisi pia tukachelewa katika maendeleo kwa ajili hiyo, kwamba ilikuwa ni mahali pamewekwa kidogo kwa ajili ya 'kanyanga'. Kwa hiyo, tunaomba historia hizi wakati huu Tanzania ni Mwenyekiti zikae sawa, kila mtu apewe kipande chake anachokistahili. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya ya kupongeza sana nafasi yetu katika SADC tumefikia mwisho wa shughuli zetu za leo, *immediately* baada ya hapa nawaomba wote tuelekee Ukumbi wa Msekwa ili tufanye *briefing* fupi, wale wanaojisikia kupita *canteen* pia wanaweza kupita dakika tano pale ili tukimaliza *briefing* basi jioni tuwe na uhuru.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Hatuwezi kuyamaliza kwenye *briefing* hayo ya mwongozo na nini?

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, hiyo ni muhimu.

SPIKA: Haya, naruhusu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Natumia Kanuni ya 68(7) sitoisoma. Ninaomba mwongozo

wako kama inaruhusiwa ndani ya Bunge Mbunge kutoa *data* au taarifa ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Agness Marwa wakati anachangia amesema kwamba Mheshimiwa Neema Mgaya ambaye ndiyo mimi, nilitoa vyerehani kumi kwa ajili ya kuanzisha viwanda, ilhali ulimwengu mzima unajua nilitoa vyerehani 370 vyenye thamani ya milioni 90 nikaanzisha viwanda vidogo vidogo kwa wanawake wa Mkoa wa Njombe. Hivyo basi, ninapenda arekebishe *statement* yake ili isomeke sahihi kwenye *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Kicheko/Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Naona hamtofautiani, umeweuka sawa *record* kwa hiyo Mheshimiwa Neema umeiweka *Hansard* sawa, naomba *Hansard* isomeke hivyo, ujumbe wenu ni mmoja tunakupongeza sana na Waheshimiwa Wabunge wengine tuige utaratibu huo wa kuwakumbuka wapiga kura wetu kama alivyofanya Mheshimiwa Neema Mgaya, tunakupongeza sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapa naomba sasa Waheshimiwa Wabunge nahirishwa shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu Kamili Asubuhi. Nawaomba tukitoka hapa *straight* tuende Msekwa *Hall*.

(*Saa 5.59 Asubuhi Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 4 Septemba, 2019, Saa Tatu Asubuhi*)